# UBORA WA TAFSIRI KATIKA KAMUSI TAFSIRI ZA MTANDAONI

**TASNIFU YA**

**WINNIE O. LUKUNGU**

**KATIKA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**JUNI 2024**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine

**Sahihi**............................ **Tarehe:** 10/06/2024

**WINNIE O. LUKUNGU**

C50/OL/34129/2016

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu Cha Kenyatta kwa idhini yangu kama msimamizi.

**Sahihi** 24-06-2024 **Tarehe:**............................

**DKT. BONIFACE NGUGI**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

## TABARUKU SPESHELI

*Kwa Stephen Matolo Kyalo,*

*Ni nani naambieni, ila ndiwe muhibu,*

*Waama nisemeni, kwa ombi ndiwe jawabu*

*Mtimani mesheheni, kila ndwele u tabibu*

*Umenifaa!*

*Waama ni taabani, ukiwa mbali tabibu*

*Menifaa masomoni, msaada wa karibu*

*Nizamapo mabukuni, watulia kama bubu*

*Umenifaa!*

*'Kanipeleka nyanjani, nd'o maswali kuyajibu*

*Ndiwe raha mdomoni, u zaidi ya zabibu*

*Wa milele maishani, ni wewe wangu muhibu*

*Umenifaa!*

Kwa wazazi wangu wapenzi Jane na Festus Lukungu na aila yetu yote kwa jumla: Larry, Morgan, Raydon, Caroline, Sharon na Rolland, bila kumsahau Raphael, asanteni kwa kunionyesha upendo usio kifani kwa muda wote wa masomo yangu. Kwa Pauline, sina mengi ila kukuhakikishia ule upendo wangu wa kwanza kwako hujawahi fifia. Kwa rafiki wa dhati, mwendazake Profesa Ahmed E. Ndalu, kwa kunitia shime katika maswala ya uandishi na kunifumbua macho ili kubaini uhondo uliopo katika lugha ya Kiswahili, mbali na kunitambulisha kwa wanalugha tajika nchini. Nitakuenzi daima, hadi tutakapokutana.

## SHUKRANI

Mafanikio ya kazi hii adhimu yanahusisha wengi, hivyo, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitawashukuru. Kwanza, ninamshukuru sana Mungu Mwenyezi kwa kunijalia uzima na uwezo wa kukamilisha utafiti huu kwani pasipo Rehema zake nisingeweza kukamilisha kazi hii nzito.

Pili, ninamshukuru sana Dkt. Bonface Ngugi aliyekubali kuwa msimamizi wangu katika kazi hii. Pamoja na majukumu mengi ya kitaaluma na kijamii aliyonayo, hakuchoka kuniongoza na kunitia moyo katika kipindi chote cha kazi hii ya utafiti. Busara, uvumilivu na juhudi zake za dhati kwangu zimefanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Tatu, ninawashukuru wahadhiri wangu wa kozi mbalimbali za Kiswahili, Dakari Pamela Ngugi ambaye alikuwa mwenyekiti wa Idara, Daktari Onyango, Daktari Osore, Daktari Chacha, Daktari Gakuo na Daktari Kaui, Profesa King'ei bila kumsahau Daktari Oteyo aliyenielekeza kupitia kozi ya Utafiti. Mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, kwa kuwa kielelezo chema kwa wasomi limbukeni kama mimi, ninayetapatapa bado katika bahari hii ya usomi nikitafuta mashiko.

Kisha, shukrani zangu ziwaendee watafitiwa wote ambao walikubali kushiriki katika utafiti huu na kutoa data zilizotumika pamoja na wanafunzi wenzangu tukioshirikiana darasani wakiwa ni Lucy, Selesio, Harriet, Onesmus na Gitari bila kumsahau bibiye Beatrice kwa mwelekezo wake wa kipekee. Namshukuru Bwana Mutugi Charles, naibu wa mwalimu mkuu shuleni Kangundo kwa msaada wake wa kipekee.

Mwisho, ninawashukuru wengine wote waliosaidia kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha kukamilika kwa utafiti huu, ambao hawako katika makundi tajwa hapo juu.

## ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| **A.C** | Aligned Corpus, Kongoo iliyolainishwa |
| **D.C** | Dictionary Compiler (Programu ya kuandaa kamusi) |
| **LC** | Lugha Chanzi |
| **LL** | Lugha lengwa |
| **MC** | Matini Chanzi |
| **ML** | Matini Lengwa |
| **SALAMA DC** | Programu ya SALAMA ya kuandaa kamusi kwa kutumia kongoo (Dictionary Compiler) |
| **TUKI** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| **NACOSTI** | The National Commission for Science Technology And Innovation |
| **KU** | Kenyatta University |
| **KIKO** | Kiswahili kwa Kompyuta |
| **KICD** | Kenya Institute of Curricullum Development (Taasisi Ya Kenya ya kuandaa Mtaala) |
| **M.K** | Mtandao wa Kijamii |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Googles** | Mojawapo ya injini pekuzi katika mtandao ya kampuni ya kampuni ya Helinski. |
| **Kamusi** | Kitabu chenye maneno ambayo hupangwa kialfabeti huku yakitolewa maana na matumizi yake. |
| **Kongoo/Kopasi** | Mkusanyiko wa maneno yaliyokusanywa na kuhifadhiwa kama yameainishwa au katika hali yake halisi ya kimatumizi. |
| **Lugha** | Mtindo atumiao mtu kujieleza kama vile Kiswahili. |
| **Maana** | Kiashiria kinachotokana na neno. |
| **Mawasiliano** | Upashanaji wa habari kwa njia mbalimbali. |
| **Mradi** | Mpangilio fulani wa maendeleo. |
| **Rununu** | Simu tamba. |
| **SALAMA DC** | Programu ya SALAMA ya kuandaa kamusi kwa kutumia kongoo (Dictionary Compiler). |
| **Tafsiri** | Ubadilishaji wa neno kutoka lugha moja hadi nyingine. |
| **Tarakilishi** | Mashine ya kuhesabu, kupanga au kuchanganua data. |
| **Opera mini** | Programu ya kuchakura mtandaoni. |
| **Google Go** | Programu ya kuchakura mtandaoni. |
| **Chrome** | Programu ya kuchakura mtandaoni. |
| **Sakura** | Kutafuta maelezo mtandaoni. |

## IKISIRI

Kiswahili ni lugha inayozidi kukita mizizi kidijitali kupitia mbinu anuai ikiwemo programu za kamusi na vitabu vingine kama Bibilia vilivyoswahilishwa na kuhifadhiwa mtandaoni. Utafiti huu ulinuia kudihirisha ubora wa tafsiri ya maneno yaliyotolewa katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Kwa kuwa enzi hii kuna watumizi wengi wa mtandao kwa malengo anuai, kamusi za mtandaoni zina dhima kuu na hivyo kuwepo na tafsiri potovu kunaweza kuwaathiri watumiaji wengi. Utafiti ulichukua muundo wa kutathmini tafsiri ya maneno kwenye kamusi zilizoteuliwa za mtandaoni kuanzia alfabeti A – M na kutoa mapendekezo ya tafsiri bora zaidi, kwa msaada wa wataalamu wa lugha kama vile waandishi wa kamusi kama walivyolengwa na mtafiti. Mtafiti alishirikiana moja kwa moja na wataalamu hawa kama vile waandishi wa vitabu mbalimbali na wanaotumia kamusi hizi katika kuandaa tasnifu yake kupitia kwa mahojiano, hojaji pamoja na mawasiliano ya kila mara kupitia simuni ili kuhakikisha kuwa malengo yake yametimia. Utafiti huu ulilenga tafsiri ya Kiingereza-Kiswahili na wala sio lugha zingine. Mihimili ya Nadharia ya Isimu Kongoo ilitumika katika kupendekeza kongoo matini bora inayotumika kama tafsiri kwa kamusi za mtandao. Mbali na nadharia hii, nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo ambayo ni mojawapo ya miavuli ya nadharia ya Tafsiri ilitumika katika kuasisi tafsiri bora kwa maneno. Utafiti ulikuwa wa kimaelezo, na usampulishaji wa kimakusudi ulitumika katika kuwateua wahojiwa pamoja na kuteua data kutoka kwenye kamusi za mtandao. Data ilichanganuliwa kwa mwongozo wa mihimili ya nadharia pamoja na malengo ya utafiti. Baada ya kuchanganua data, matokeo yaliwasilishwa kwa kutumia maelezo na michoro ya jadwali kisha kutolewa maelezo yake. Matokeo ya utafiti yananuia kuboresha tafsiri ya kamusi kwenye mtandao ili kuwafaidi wategemezi, waunfaji na watumiaji wa kamusi hizi katika shughuli zao anuai. Baadhi ya watakaoweza kufaidi kwa kamusi yenye tafsiri bora ni pamoja na wasomi, watafsiri, walimu, pamoja na wageni wanaotumia kamusi hizi ili kujifundishia lugha ya Kiswahili.

## ABSTRACT

Kiswahili is a language that is progressively developing its roots in the digital world through various means including e-books such as Dictionary and Bible Applications. This study seeks to recommend and provide better translation for the words translated in the dictionaries. Since there are many internet users in this era for various needs the online dictionaries play a key role therefore having a mistranslated word in these e-books will mislead many of these users. The research will evaluate translations based on his research samples for words across alphabets A-M while recommending better words with the assistance of language experts such as dictionary writers targeted by the researcher. The researcher will incorporate these experts in the report through the use of questionnaires and interviews as well as one on one communication through phone calls to ensure the research objectives are met. The research will also target English-Swahili translators and not any other language. The constructs of The Corpus Theory will guide the research in studying the suitability of the corpus that is used as translation for the online dictionaries. Apart from this theory, the structural comparative theory, an umbrella of the Translation Theory will be used in the study to evaluate better translation for the words. The research will take a qualitative approach since explanation of the research findings befitting better translation will be in form of words. Purposive sampling will take place in the sampling of the respondents as well as in selecting words in the online dictionaries and which will be analyzed in relation to the tenets of the research theories and objectives. After analyzing data, the findings will be presented by explanations and tabulation and the research summary will be given in conclusion. These findings aim at assisting in having better translation and benefit the users of the dictionaries in their various activities. Some of those who will benefit from the dictionary with better translation include learners, translators, teachers as well as foreigners using these dictionaries to learn Swahili language.

## YALIYOMO

**UNGAMO** .......... **ii**

**TABARUKU SPESHELI** .......... **iii**

**SHUKRANI** .......... **iv**

**ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU** .......... **v**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI** .......... **vi**

**IKISIRI** .......... **vii**

**ABSTRACT** .......... **viii**

**YALIYOMO** .......... **ix**

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... **xv**

**ORODHA YA VIELELEZO** .......... **xvii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** .......... **1**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 4

1.3 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.4 Malengo ya Utafiti .......... 5

1.5 Upeo na Mipaka .......... 5

1.6 Sababu za Kuchagua Mada .......... 6

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 7

1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nafasi ya Kiswahili kwenye Tarakilishi .......... 8

1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Tafsiri na Makosa Yanayaoathiri Ubora wa Tafsiri .......... 9

1.7.3 Tafiti Bayana kuhusu Makosa Yanayoathiri Ubora wa Tafsiri ............12
1.8 Misingi ya Kinadharia ....................................................................13
1.8.1 Nadharia ya Isimu Kongoo ................................................................14
1.8.2 Nadharia ya Tafsiri ya Ulinganifu wa Kimuundo ................................15
1.9 Mbinu za Utafiti ..........................................................................16
1.9.1 Sampuli ...........................................................................................16
1.9.2 Mbinu za Ukusanyaji Data ...................................................................20
1.9.3 Umuhimu na Utegemezi wa Vifaa vya Utafiti .....................................22
1.9.4 Uchanganuzi wa Data .........................................................................22
1.9.5 Uwasilishaji wa Matokeo ....................................................................23
1.9.6 Maadili ya Utafiti...............................................................................23
1.10 Hitimisho ..........................................................................................24
**SURA YA PILI: TAFSIRI POTOVU KATIKA KAMUSI TAFSIRI ZA MTANDAONI ........................................................................................25**
2.0 Utangulizi ...........................................................................................25
2.1 Tafsiri Potovu katika Kamusi za Mtandaoni ..............................................25
2.1.1Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti A....................................26
2.1.2 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti B ...................................28
2.1.3 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti C ...................................29
2.1.4 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti D...................................31
2.1.5 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti E ...................................32

2.1.6 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti F ....................................34

2.1.7 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti G ....................................36

2.1.8 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti H ....................................37

2.1.9 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti J .....................................39

2.1.10 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti L ..................................41

2.1.11 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti M .................................43

2.2 Hitimisho ...............................................................................................44

**SURA YA TATU: VYANZO VYA TAFSIRI POTOVU KATIKA KAMUSI TAFSIRI ZA MTANDAONI ...............................................................46**

3.0 Utangulizi ..............................................................................................46

3.1 Vyanzo vya Tafsiri Potovu katika Kamusi Tafsiri za Mtandaoni ...............46

3.1.1 Tofauti za Muundo wa Lugha ya Kiswahili na Muundo wa Lugha ya Kiingereza ..............................................................................47

3.1.2 Tofauti za Kimitindo Kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza ........48

3.1.3 Matatizo Ya Uteuzi Wa Msamiati/Maneno Maalum............................50

3.1.4 Matatizo Katika Kiwango Cha Uhawilishaji ........................................51

3.1.5 Udurusu wa Kongoo- Matini Kutofanyika au Kufanyika Kiholela......52

3.1.6 Kutokuwepo Kwa Sera Za Kuhakikisha Uboreshaji Wa Kamusi-Tafsiri Za Mtandaoni Mara Kwa Mara ................................................53

3.1.7 Kutokuwa kwa Sera ya kuhakiki na kusawazisha Kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao .....................................................54

3.1.8 Upana Wa Maneno Na Kuzuka Kwa Misamiati Ya Kiingereza Na Kiswahili ....................................................................................56
3.1.9 Swala La Lugha Ya Kiswahili Kukua .................................................57
3.1.9 Makosa ya kiufundi; kikagua tahajia..................................................58
3.1.10 Makosa Kutokana na Hali/ Mambo Mengineyo.................................59
3.2 Viwango Anuai vya Makosa Vilivyoathiri Ubora Wa Tafsiri ....................59
3.2.1 Makosa Katika Kiwango cha Mofolojia..............................................59
3.2.2 Makosa Katika Kiwango Cha Semantiki.............................................61
3.2.3 Makosa katika Kiwango cha Pragmatiki .............................................62
3.3 Hitimisho ..................................................................................................63
**SURA YA NNE: MIKAKATI YA KUBORESHA KAMUSI-TAFSIRI ZA MTANDAONI ..................................................................................65**
4.0 Utangulizi .................................................................................................65
4.1 Mikakati Iliyojitokeza ya Kuboresha Kamusi-Tafsiri za Mtandaoni ..........65
4.1.1 Kubuniwa Kwa Sera ya Kuhakiki Kamusi-tafsiri za Mtandaoni .........66
4.1.2 Udurusu wa Kongoo- Matini Kufanywa kwa Ufasaha.........................68
4.1.3 Kujumuisha Wataalamu Wa Lugha Katika Maandalizi Ya Kongoo-Matini ..........................................................................................69
4.1.4 Ujumuishaji Wa Maneno Mapya Mara Kwa Mara ..............................70
4.1.5 Ujumuishaji Wa Idara Ya Lugha Vyuoni Katika Kuandaa Kongoo Matini ..........................................................................................72

4.1.6 Udurusu Wa Kamusi –Tafsiri Mitandaoni Kufanywa Mara Kwa Mara ........................................................................................73

4.1.7 Kutathmini Utendakazi Wa Kikagua Tahajia Mara Kwa Mara ...........74

4.1.8 Kuongeza Nguvu-Kazi Ya Wahariri ...................................................76

4.2 Hitimisho ..........................................................................................77

**SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ......................................................................................................78**

5.0 Utangulizi ..........................................................................................78

5.2 Muhtasari wa Utafiti...........................................................................78

5.3 Matokeo ya Utafiti..............................................................................79

5.3.1 Kubainisha Tafsiri Potovu katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni ..........80

5.3.2 Vyanzo vya Tafsiri Potovu kwenye Kamusi za Mtandaoni .................80

5.3.3 Mikakati ya kuboresha tafsiri bora inayoweza kutumika katika kamusi za mitandaoni ..............................................................................81

5.4 Mapendekezo ya Utafiti .....................................................................82

5.5 Hitimisho ..........................................................................................84

**MAREJELEO ..........................................................................................85**

**VIAMBATISHO .......................................................................................87**

Kiambatisho I: Fomu Ya Kushiriki Utafiti Kwa Hiari.....................................87

Kiambatisho II: Hojaji Kwa Watumiaji Wa Kamusi-Tafsiri ............................88

Kiambatisho III: Hojaji Kwa Mtaalamu Wa Teknolojia..................................90

Kiambatisho IV: Barua Ya Chuo Ya Ruhusa Ya Utafiti....................................92

Kiambatisho V: Idhini Ya NACOSTI .................................................................93

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 1.1: Watafiti wote Kwa Jumla ... 19

Jedwali 1.2: Sampuli ya Utafiti ... 19

Jedwali 1.3: Jinsi ya kupata Sampuli katika Jumuiya ... 20

Jedwali 2.1: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti A ... 26

Jedwali2.2: Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti B ... 28

Jedwali 2.3: Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti C ... 30

Jedwali 2.4: Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti D ... 31

Jedwali 2.5: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti E ... 33

Jedwali 2.6: Tafsiri Potovu ya Maneno kwenye Alfabeti F ... 34

Jedwali 2.7: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti G ... 36

Jedwali 2.8: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti H ... 38

Jedwali 2.9: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti J ... 40

Jedwali 2.11: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti M ... 43

Jedwali 3.1: Tofauti Za Muundo Wa Lugha Ya Kiswahili Na Muundo Wa Lugha Ya Kiingereza ... 47

Jedwali 3.3: Matatizo Ya Uteuzi Wa Msamiati/Maneno Maalum ... 50

Jedwali 3.4: Matatizo Katika Kiwango Cha Uhawilishaji ... 51

Jedwali 3.5: Udurusu wa kongoo – matini kupuuzwa au kufanyika koholela ... 52

Jedwali 3.6: Kutokuwepo Kwa Sera Za Kuhakikisha Uboreshaji Wa Kamusi-Tafsiri Za Mtandaoni ... 54

Jedwali 3.7: Kutokuwa Kwa Sera Ya Kuhakiki Na Kusawazisha Kongoo Ya Kiswahili Na Ya Kiingereza Kwenye Mtandao ... 55

Jedwali 3.8: Maneno Ya Kiingereza Yasiyo Na Tafsiri Sambamba Ya Kiswahili 56

Jedwali 3.9: Swala La Lugha Ya Kiswahili Kukua ............................................... 57
Jedwali 3.10: Tafsiri potovu kutokana na makosa ya kiufundi.............................. 58
Jedwali 3.11: Makosa Katika Kiwango Cha Mofolojia......................................... 60
Jedwali 3.12: Makosa katika kiwango cha Semantiki ........................................... 61
Jedwali 3.13: Makosa Katika Kiwango Cha Pragmatiki ....................................... 63
Jedwali 4.2: Udurusu Wa Kongoo- Matini Kufanywa Kwa Ufasaha..................... 68
Jedwali 4.3: Kujumuisha Wataalamu Wa Lugha Katika Maandalizi Ya Kongoo-Matini ........................................................................................ 69
Jedwali 4.4: Ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara ........... 71
Jedwali 4.5: Ujumuishaji Wa Idara Za Lugha Ya Kiswhili Vyuoni Katika Kuandaa Kongoo Matini ..................................................................... 72
Jedwali 4.6: Udurusu Wa Kamusi-Tafsiri Ya Mitandaoni Kufanywa Mara Kwa Mara ......................................................................................... 74
Jedwali 4.7: Kutathmini Utendakazi Wa Kikagua Tahajia Mara Kwa Mara ......... 75
Jedwali 4.8: Kuongeza Nguvu-Kazi Ya Wahariri.................................................. 76

## ORODHA YA VIELELEZO


Kielelezo 2.1: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti A katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni ........................................................ 27

Kielelezo2.2: Tafsiri Potovu Ya Neno 'Busy' Kwenye Alfabeti B Katika Kamusi-Tafsiri Ya Mtandaoni .......................................... 29

Kielelezo 2.3-kina mfano wa tafsiri potovu ya neno 'Drive' kwenye alfabeti D katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni ................................ 32

Kielelezo 2.4: Tafsiri Potovu ya Neno 'envying' kwenye Alfabeti E katika Kamusi-tafsiri ya Mtandaoni............................................. 34

Kielelezo 2.5: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti F katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni........................................................ 35

Kielelezo 2.6: Tafsiri Potovu Cha neno 'glow' kwenye Alfabeti G Katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni ambayo imetafsiriwa kama Mwanga katika Kiswahili. ................................................ 37

Kielelezo 2.7: Tafsiri Potovu Cha neno 'humiliate' kwenye Alfabeti H Katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni .................................. 39

Kielelezo 2.8: Tafsiri Potovu Cha neno 'humiliate' kwenye Alfabeti J Katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni............................................. 41

Kielelezo 2.9: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti L katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni........................................................ 42

Kielelezo 2.10: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti M katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni........................................................ 44

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Misamiati ya Kiswahili imeingizwa katika vyombo vingi vya kiteknolojia kama vile simu, tarakilishi na mitambo ya pesa benkini ili kutimiza malengo yao anuai. Ili kutimiza malengo ya mawasiliano katika vyombo hivi, tafsiri za istilahi na programu mbalimbali ulifanyika ili kufaidi wapenzi wa Kiswahili na wale wasioielewa lugha ya Kiingereza kama inavyotumika katika hivi vyombo. Teknolojia ya karne hii vile vile imewezesha kuibuka kwa programu zinazowezesha uhifadhi wa vitabu katika mtandao na kurahisisha shughuli ya usomaji na utafiti. Katika baadhi ya vitabu vya sarufi vilivyohifadhiwa kwenye mtandao ni kamusi, ili kuwezesha wasomi, watafiti na watumiaji wa mtandao kufaidika kutoka kutokana nazo.

Kamusi ni kitabu chenye maneno ambayo hupangwa kialfabeti huku yakitolewa maana, aina na matumizi yake (Kamusi Teule ya Kiswahili, 2013.) Kulingana na Waihiga na Wamitila (2003), kamusi ni kitabu kinachohifadhi maneno yanayopatikana katika lugha fulani katika wakati fulani, na hueleza maana ya maneno hayo kwa njia inayoeleweka na watumiaji wa lugha hiyo pamoja na wanaojifundisha lugha inayohusika. Pia, Waihiga na Wamitila wanaeleza umuhimu wa kamusi, kwamba hufafanua maana ya maneno mbalimbali na kueleza jinsi maneno hayo yanavyoandikwa na kuendelezwa. Wanazidi kufafanua umuhimu wa kamusi kama vile kutoa maelezo au taarifa kuhusiana na ngeli za nomino zinazopatikana katika lugha mbali na kueleza jinsi ya kutamka na kutumia maneno fulani na pia kujua visawe na vitawe vya maneno.

Kwa mujibu wa Waihiga na Wamitila (2013), kuna aina nyingi za kamusi zilizowekwa katika vitengo mbalimbali kama vile kutegemea walengwa, kwa mfano kamusi za wanafunzi wa shule za msingi au za upili. Kuna kamusi kulingana na eneo au mawanda kama vile kamusi ya sayansi au kamusi ya fasihi, na kamusi kulingana na idadi ya lugha zinazohusika. Katika kitengo cha idadi ya lugha, kuna kamusi wahidiya ya lugha moja, na kamusi thaniya ya lugha mbili. Swala la kuwa na kamusi ya lugha mbili ni kazi halisi ya tafsiri, kwani kamusi hizi hutoa tafsiri za maneno ya lugha moja hadi nyingine (Waihiga, 2013).

Katika kazi hii, tafsiri inachukua nafasi kubwa sana kwani tunatathmini ubora wa maneno yaliyotolewa kama tafsiri ya maneno ya Kiingereza. Tafsiri ni neno la asili ya Kiarabu, na lenye maana ya kutoa maana ya maneno kutoka lugha moja hadi lugha nyingine au kutoa andiko au maelezo fulani katika lugha nyingine kwa maana ile ile (TUKI, 2006). Kulingana na Newman (1982), tafsiri ni jaribio la kuwasilisha ujumbe ule ule ulioandikwa katika lugha moja kwa lugha nyingine. Mwan'sonko na wenzake (2006) nao wanaeleza tafsiri kama zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa mujibu wa Catford (1965), tafsiri ni zoezi la kuchukua mawazo yaliyo katika maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzi) na kuweka badala yake mawazo yanayolingana katika lugha nyingine (lugha lengwa). Kamusi za thaniya zimeweza kuhifadhiwa katika mtandao kwa njia ya kongoo ili kutoa tafsiri za maneno katika lugha mbalimbali.

Tafsiri tunayoangazia katika tasnifu hii ni ile inayojitokeza katika kamusi za mtandaoni tu. Mtandao ni mfumo wa mawasiliano utumiao tarakilishi, simu au vifaa vingine vya kielektroniki. (Kamusi Teule ya Kiswahili, 2013) Tafsiri mtandaoni

huweza kujitokeza kupitia kwa injini pekuzi za mtandaoni mbali na kamusi mahususi za tafsiri kama vile *The English-Swahili Offline Translator*. Tafsiri za maneno hutolewa kwa kutoa maana ya maneno kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa. Katika tafsiri hii, aina ya neno haipewi kipaumbele wala matumizi yake katika sentensi kama kamusi za kawaida zilizochapishwa, maana hutolewa tu kwa njia ya moja kwa moja.

Kwa vile tasnifu hii inaangazia tafsiri za kamusi za mtandaoni kwa kutathmini ubora wa tafsiri hizi, ni jambo la muhimu sana kuangazia maana za maneno hayo katika lugha chanzi na lugha lengwa. Dhana ya maana imejaribu kuelezwa kupitia kwa nadharia tofauti tofauti (Ullman, 1964). Nadharia ya kwanza ni ile inayoichukulia maana ya neno kama kitajwa au kiashiriwa. Kwa mujibu wa nadharia hii, maana ya neno ni ule uhusiano uliopo baina ya neno na kile kilichukusudiwa. Nadharia ya pili ni ile inayoichukulia maana ya neno kama dhana. Nadharia hii inadai kuwa maana ya neno ni dhana ambayo msemaji au msikilizaji anaipata kutokana na kile kilichokusudiwa. Nadharia nyingine ni ile inayodai kuwa maana ya neno inatokana na jinsi neno hilo linavyotumika katika jamii ya wanalugha fulani (Ullman 1964). Nadharia hizi husaidia kujua maana ya maneno, na nadharia ya tafsiri inatueleza kuwa njia moja ya kujua maana ni kutafsiri neno hilo.  Iwapo tafsiri potovu itatumika, makosa ya maana yanaweza kutokea katika muktadha ambamo neno hilo limetumika (Richard, 1999). Mada yetu basi ilizaliwa ili kutathmini ubora wa tafsiri katika kamusi-tafsiri za mtandaoni ili kujaribu kukwepa tafsiri potovu kwa maneno ya Kiingereza.

## 1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kutathmini ubora wa tafsiri katika kamusi- tafsiri za mtandaoni. Tafiti za awali kama vile; Kahigi (2005) aliyechunguza makosa ya kisintaksia katika makala magazetini na Mabeya (2012) aliyetafiti kuhusu uzalishaji wa msamiati katika mradi wa *Microsoft East Africa* 2004-2009 hazikujishughulisha na suala hili. Hivyo basi, kadri mtafiti ajuavyo, hakuna tafiti za awali ambazo zimefanywa kuhusu ubora wa tafsiri katika kamusi-tafsiri za mtandaoni ilhali kamusi-tafsiri za mtandaoni zinategemewa na watumizi wengi katika kazi zao za kutafsiri.

Utafiti huu ulichochewa na tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Kwa mfano, kwa kuzingatia kanuni za tafsiri, iwapo neno la Kiingereza la kutafsiriwa ni kitenzi, basi tafsiri yake lazima ijitokeze kama kitenzi wala neno lisinominishwe. Tafsiri ya baadhi ya maneno ya Kiingereza katika Kiswahili kwenye kamusi-tafsiri za mtandaoni inaonekana kutozingatia kanuni za tafsiri na hivyo basi kutilia shaka ubora wa tafsiri hiyo. Tafsiri kama hiyo potovu inaweza kuwapotosha wategemezi wakamusi-tafsiri za mtandaoni.

Utafiti huu umechunguza baadhi ya maneno yaliyotafsiriwa visivyo kwa kutozingatia kanuni za kutafsiri au maneno hayo yanapotumiwa kwenye sentensi maana halisi huweza kupotea wakati tafsiri hizo zinatumika katika muktadha maalum. Kwa kuwa utafiti huu huwezi kuandaa kongoo upya kwenye kamusi hizi, utafiti umetoa mapendekezo ambayo yanaweza kuzingatiwa katika kuandaa kamusi-tafsiri bora za mtandaoni.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

a) Je, kuna tafsiri potovu katika kamusi za mtandaoni?

b) Je, vyanzo vya tafsiri potovu kwenye kamusi- tafsiri za mtandaoni ni vipi?

c) Ni mikakati gani inayoweza kuboresha tafsiri inayotumika katika kamusi-tafsiri za mitandaoni?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kutimiza malengo yafuatayo:

a) Kubainisha tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni.

b) Kujadili vyanzo vya tafsiri potovu kwenye kamusi za mtandaoni.

c) Kupendekeza mikakati ya kuboresha tafsiri bora inayoweza kutumika katika kamusi hizi.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Vyombo vya kiteknolojia ni vya vitengo mbalimbali kulingana na mazingira ambamo matumizi yake yanahitajika kwa mfano mazingira ya hospitalini, nyumbani na ofisini. Vyombo hivi ni kama vile tovuti, televisheni, redio, setelaiti, simu na tarakilishi. Utafiti ulishughulikia vifaa vya simu na tarakilishi tu.

Ijapokuwa tayari tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika teknolojia, bado kuna haja ya kushughulikia matumizi ya kamusi katika vifaa vya kiteknolojia. Hivyo basi, utafiti huu ulizingatia matumizi ya kamusi katika vifaa vya simu na tarakilishi.

Kamusi za kitafsiri ni za aina nyingi, vilevile hushughulikia lugha anuwai, kama vile Kiingereza, Kijerumani, Kichina, na kadhalika. Utafiti wetu lakini umejikita katika kamusi za uwili-lugha tu, na haswa kamusi za Kiingereza- Kiswahili wala si lugha nyingine. Pia, kamusi ambazo tulishughulikia ni zile za:

a) The English-Swahili Translator,

b) Offline English –Swahili Dictionary

c) English- Swahili online Translator.

Viwango vinne vikuu vya lugha kulingana na wanaisimu ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki (Richard, 1999). Fonolojia hushughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumika katika lugha fulani, mofolojia huchunguza maumbo ya maneno, semantiki ni taaluma inayojihusisha na maana katika lugha na sintaksia huchunguza na kufafanua mpangilio na uhusiano wa maneneo katika sentensi (TUKI). Utafiti huu ulijikita Katika viwango hivi vinne kwa kuzingatia foni, mofimu na maneno yanachangia katika kujenga vipashio vya maneno yenye maana.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Upotovu katika tafsiri huweza kubainika katika njia tofauti tofauti, kama vile maongezi ya kawaida ya watu, maandishi ya jumla, kazi za kiakademia, na kazi za wanafunzi. Mada hii ya Ubora wa Tafsiri katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni itawezesha washika dau hawa kupevuka na kuwa makini zaidi katika maandishi, maongezi, au kazi zao ili kuepuka makosa haya. Kwa mujibu wa Jilala (2014), tafsiri ni mchakato ambao hufuata kanuni fulani na sharti ifanywe hatua kwa hatua ili iwe bora.

Mada hii ya Ubora wa Tafsiri katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni pia inaoana na enzi hii ya utandawazi ambapo kunabuniwa misamiati katika nyanja mbalimbali inayoingizwa katika programu za tarakilishi ili kukidhi mahitaji ya watumizi wa lugha. Matumizi ya mtandao ndiyo mbinu inayotumika kama hifadhi ya taarifa, vitabu na kila habari ambayo inayohitajika katika uwanja wowote ule, pamoja na mbinu za kusoma kama vile elimu masafa kujipatia manufaa kupitia teknolojia hii. Kihore (2002) anaeleza kuwa kuingizwa kwa lugha ya Kiswahili katika programu za tarakilishi na kuwekwa mtandaoni kunasaidia watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuchanganua data katika lugha ya Kiswahili badala ya lugha ya Kiingereza, na hivyo kutupa sababu ya kuchagua mada hii.

Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ina hadhi ya kimataifa, (Ipara, 2008), kuna haja ya kuhakikisha kuwa lugha hii inasambazwa kwa ufasaha wake. Hili litaepusha kupotosha wasiojua lugha hii na wanaotegemea simu na tarakilishi kujifunza au kuitumia lugha hii kwa njia moja au nyingine. Mwisho, iwapo neno litatafsiriwa visivyo, basi maana yake itapotea na lengo la mawasiliano halitaafikiwa.

**1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Usomaji wa vitabu, tasnifu na makala mbalimbali ulidhihirisha kuwa kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu tafsiri ambazo zinahusiana na utafiti huu. Hata hivyo, kwa vile uwanja wa tafsiri ni mpana, masuala yanayoshughulikiwa na tafiti mbalimbali hutofautiana. Kwa sababu hiyo, kuna mambo mengineyo yanahitaji kutafitiwa ili kutoa mchango na kuziba pengo ambalo limeachwa na tafiti zilizotangulia.Lengo kuu la sehemu hii ni kuonyesha uhusiano uliopo kati ya tafiti zilizofanywa na kazi hii na vile vile kuonyesha pengo linalofaa kuzibwa.Tafiti hizo zilishughulikiwa katika sehemu tatu kuu kama ifuatavyo:Yaliyoandikwa kuhusu

nafasi ya Kiswahili kwenye tarakilishi, yaliyoandikwa kuhusu taaluma ya tafsiri na makosa katika tafsiri na tafiti bayana kuhusu makosa yanayoathiri ubora wa tafsiri.

### 1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nafasi ya Kiswahili kwenye Tarakilishi

Wataalamu mbalimbali wa lugha wametafiti kuhusu nafasi ya Kiswahili katika tarakilishi. Mawazo yao yalitufaa katika utafiti huu kwani ulichunguza ubora wa tafsiri kama inavyojitokeza kwenye vyombo vya simu na tarakilishi. Baadhi ya tafiti hizi zililenga kubaini matumizi ya lugha ya Kiswahili katika tarakilishi tofauti na utafiti huu uliolenga kubaini tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni.

Mabeya (2009) ameangazia matumizi ya Kiswahili katika mradi wa *Microsoft East Africa*na kubainisha mbinu zilizohusika katika uundaji wa msamiati katika mradi huu. Kupitia kwa utafiti huu tuliona jinsi mbinu za uundaji wa misamiati iliyohifadhiwa kama kongoo-matini na inayotumika kama tafsiri kwa maneno inavyoathiri ubora wa tafsiri.

Kihore, (2002) anaeleza kuhusu kuingizwa kwa Kiswahili katika mfumo wa kompyuta ili kumpa mtumiaji wa kompyuta uhuru wa kutumia Kiswahili badala ya Kiingereza. Programu kwenye kompyuta zilizoswahilishwa zinawezesha watumizi kuchanganua na kuwasilisha matokeo ya data kwa Kiswahili kwa mujibu wa utafiti huu, na tasnifu hii ilichunguza ubora wa kongoo matini inayotumika kama tafsiri.

Kahigi, (2007) anaeleza kanuni za uundaji wa istilahi katika tarakilishi ambazo waundaji walizikubali katika uundaji huo. Utafiti huu umetufaa kwani baadhi ya istilahi hizi zimetokana na tafsiri. Hata hivyo, utafiti huu haukulenga mbinu zinazotumika katika uundaji wa istilahi kwa kina lakini ulionyesha namna tafsiri za

misamiati zilizojumuishwa katika kongoo-matini zilivyo na dosari na kupendekeza tafsiri bora. Huu ndio utafauti kati ya kazi hii na kazi yangu.

Kutokana na haya, ni bayana kuwa mengi yameandikwa kuhusu nafasi ya Kiswahili katika tarakilishi nayo yalitufaa sana katika utafiti wetu utakaohusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika programu za kamusi kwenye vyombo vya kiteknolojia vya simu na tarakilishi pia.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Tafsiri na Makosa Yanayaoathiri Ubora wa Tafsiri

Zipo tafiti zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali kuhusiana na taaluma ya tafsiri na yatakayotufaa katika utafiti huu. Wataalamu hawa ni kama vile Ali (1981), Omboga (1986), Shitemi (1990), Kaviti (2005), Nyaga (2009) Simiyu (2010) na Mutugi (2012) na ambao tuliangazia tafiti zao. Nyingi ya tafiti hizi zililenga kubaini makosa, changamoto na matatizo wanayoyapitia wafasiri katika mchakato wa kutafsiri makala ya kuchapisha ilhali kazi hii ililenga kubaini tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni ambapo changamoto za kiteknolojia zinaibuka.

Ali, (1981), alijadili makosa mbalimbali ambayo hutokea katika taarifa za habari zilizotafsiriwa katika Idhaa ya Sauti ya Kenya, akizingatia jinsi ambavyo mawasiliano mazuri hupotoshwa na makosa kama hayo. Mchango wake ulikuwa muhimu, hasa tunapozingatia matatizo ya tafsiri potovu katika mtandao, na jinsi tafsiri hii inavyoweza kupotosha mawasiliano mazuri.

Kaviti, (2005), amechunguza makosa ya kisintaksia yanayojitokeza kwenye tafsiri za makala ya magazetini, akitumia nadharia ya tafsiri mawasiliano kwenye utafiti wake. Ameonyesha upungufu uliopo kwenye makala yaliyotafsiriwa, huku

akisisitiza umuhimu wa kusawazisha sintaksia ndipo maana ya ujumbe asilia umfikie msomaji. Anashauri kuwa muundo wa sentensi wa LL uongoze tafsiri na kuwe na matumizi ya miundo ya kisintaksia inayokubalika. Ameshughulikia vipengele kama vile virai, vishazi, dhamira na toni, njeo na hali. Kaviti anashughulikia tafsiri kwa kuzingatia vipengele vya kisintaksia. Utafiti huu ni nguzo haswa tulipozingatia neno lililotafsiriwa katika muktadha wa sentensi.

Mutugi (2012) amechunguza changamoto zinazoibuka katika kutafsiri pronomino za Kiingereza hadi Kiswahili na ameonyesha kwamba kupotea kwa maana huibuka kwa sababu ya tafsiri mbovu. Kwenye uchunguzi wake anasema tafsiri ni mradi unaohusu masuala kadhaa, na kila sentensi inahusu uteuzi mwingi kuhusu habari zake. Hivyo basi, tafsiri ni mchakato wala si tukio, ambapo maana huhawilishwa kutoka LC hadi kwa LL. Ni mchakato ambao mtafsiri hulazimika kuamua ni seti ipi kati ya faridi zilizopo za kileksika aitumie, njeo gani au hali inayofaa, wapi atumie kiwakilishi na wapi atumie nonimo. Kwa muhtasari anasema tafsiri huhusu maamuzi ya kiisimu yanayofanywa wakati wa kuhawilisha maana. Utafiti huu ulitufaa kwa kuwa umeshughulikia kipengele mahususi cha kiisimu kama utafiti huu ulivyofanya.

Newman, (1982) ameguzia matatizo ambayo watafsiri hukumbana nayo na njia za kuyatatua kupitia kwa matumizi ya mihimili ya kinadharia wakati wa kutafsiri. Vile vile ameorodhesha aina za tafsiri zinazotumika kulingana na aina matini, muktadha wa matini pamoja na sajili inayotumika. Kazi yake ilitoa mchango mkubwa kuhusiana na nadharia za tafsiri na dhana zinazohusika katika utafiti huu.

Nyaga, (2009) ameshughulikia ulinganifu katika tafsiri za kifasihi akitumia mwelekezo wa ‘Usaliti Mjini’. Ameonyesha mwonekano tofauti tofauti wa

ulinganifu akieleza jinsi ulinganifu unaibua changamoto katika kutoa maana. Utafiti huu ulitufaa kwani huu utafiti unajaribu kueleza ulinganifu kama chanzo cha makosa ya kitafsiri.

Omboga, (1986) alifanya utafiti unaohusu makosa ya kisarufi na jinsi ya kuyarekebisha kupitia kuwa na umilisi na matumizi ya mihimili ya nadharia inayohusiana na utafiti. Baadhi ya mapendekezo yake yatatusaidia katika kutafuta suluhu kwa makosa ya kitafsiri yanayodhihirika katika kamusi tulizoangazia. Kwa mfano, pendekezo lake la kuhusisha nadharia mahususi katika kutafsiri.

Simiyu, (2010), anasema kuwa ulinganifu wa kipragmatiki hufaulisha maana katika tafsiri. Akitumia nadharia ya umaanisho, anasema kwamba maana hupatikana kupitia vipengele vya kipragmatiki. Maoni yake yalifaa katika kuelewa umuhimu wa vipengele hivi vya kipragmatiki kwani tafsiri ya maneno, kama ilivyoangaziwa katika utafiti huu huathiri muktadha wa maneno ambamo tafsiri hiyo itatumika.

Shitemi, (1990), kwa kutumia *Wema Hawajazaliwa* kama kielelezo, ameshughulikia mambo yanayoathiri maamuzi ya ulinganifu ambamo tafsiri hufanywa huku akitumia tafsiri ya Shujaa *Okonkwo* kama kielelezo. Shitemi anaonelea kwamba tofauti baina ya matini ya lugha asilia na yale ya lugha pokezi, hutokana na sababu za uteuzi hasa kwa minajili ya kuwasiliana vyema zaidi na hadhira yake wala sio kimakosa. Utafiti huu ulitoa mwelekezo wa kujaribu kupata kiini cha makosa yanayodhihirika kwenye tafsiri za mtandao. Ni dhahiri kuwa tafiti za awali zilizohusiana na nafasi ya Kiswahili katika tarakilishi na pia zilizohusu taaluma ya tafsiri zilisalisha pengo ambalo utafiti huu unajaribu kuziba.

### 1.7.3 Tafiti Bayana kuhusu Makosa Yanayoathiri Ubora wa Tafsiri

Iribe (1996) alitafiti kuhusu Matatizo ya Leksikografia-tafsiri: Tathmini ya Kamusi ya F. Johnson (1939). Huu ni mfano wa utafiti unaohusiana kwa karibu zaidi na mada yetu ila umejikita katika kutathmini kamusi mahususi iliyochapishwa. Anaonyesha kuwa kamusi za lugha mbili zina matatizo mengi ya tafsiri katika ngazi mbalimbali za lugha, mbali na kufafanua dhana ya tafsiri huku akionyesha matatizo, umuhimu na nafasi yake. Pia, anaonyesha nafasi ya maana katika tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri-huru na tafsiri mawasiliano.

Katika utafiti huu, anazingatia aina za sarufi, na kutoa ufafanuzi wa matatizo ya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia katika kamusi za uwili lugha. Hatimaye, ametoa mifano ya tafsiri zisizo sahihi kimofolojia na kisintaksi katika kamusi ya Johnson (1939) ya Kingereza-Kiswahili. Katika tathmini hii, Mwangi pia ameijadili dhana ya semantiki, maana katika semantiki na pia matatizo ya kisemantiki katika kamusi za uwili lugha. Matatizo haya yanahusu uchaguzi wa visawe, uchanganuzi wa maana, maneno ya jamii rnoja na ufafanuzi wa kimichoro na kimifano. Hatimaye ameyaonyesha matatizo hayo kama yalivyojitokeza katika kamusi ya F. Johnson (1939). Mwisho, ameonyesha makosa ya kisemantiki katika mifano iliyotolewa na mtunzi na matatizo mengine ya jumla katika kamusi hiyo.

Tofauti na utafiti wa Iribe (1996), utafiti huu ulizingatia dhana ya ujumuishaji wa teknolojia katika kutoa tafsiri za maneno hivi kwamba tatizo la utafiti huu litatokana na hali ya tafsiri za maneno kutokana na kongoo kwenye vyombo vya simu na tarakilishi. Tafsiri basi zitakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kongoo matini pamoja na mchakato wa kijumla uliohusika katika kuandaa kongoo ya tafsiri kwenye kamusi za mtandaoni. Tofauti na utafiti wake pia, hatukujikita katika kamusi

zilizochapishwa bali katika programu mbalimbali za kamusi- tafsiri za mtandaoni na jinsi tafsiri za mtandaoni ambavyo programu hizi zinavyoweza kuboreshwa ili kuboresha tafsiri zinazotoa. Swala hili lina uzito mno kwani mchakato wa kuwa na kongoo –tafsiri inayounda vitabu vya mtandaoni kama vile kamusi unaathiri ubora au makosa yatakayojitokeza katika makala yanayotolewa kama tafsiri kwenye kamusi za mtandaoni.

Katika kujadili makosa ya kisemantiki katika kamusi za uwili lugha, Mwangi anaonyesha makosa yanayotokana na maneno ya jamii moja pamoja na ufafanuzi wa kimichoro na kimifano, ambao haukuwa kapaumbele katika utafiti huu. Badala yake, utafiti huu ulijikita katika aina za maneno zinazotolewa kama tafsiri pamoja na maumbo ya maneno hayo ambayo yanaleta makosa ya kisemantiki katika tafsiri. Kwa kuwa tafsiri kwenye kamsusi- tafsiri za mtandaoni haitoi matumizi ya maneno hayo katika muktadha wa sentensi au kufafanua maneno hayo, utafiti huu uikuwa na nafasi ya kufanya hivyo japo kwa mifano michache. Mifano hii ni kama vile maana ya maneno ambayo yana visawe vyake vinavyoweza kuhitaji ufafanuzi wa ziada.

**1.8 Misingi ya Kinadharia**

Nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kueleza hali fulani; chanzo chake, muundo wake, utenda wake na mwingiliano wake wa ndani na nje (Wamitila, 2003). Aghalabu, kila utafiti huongozwa na nadharia fulani, na utafiti huu umeangazia nadharia mbili: Nadharia ya Tafsiri, haswa mtazamo wa nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo na Nadharia ya Isimu Kongoo ambazo zimechukua nafasi muhimu katika mada ya utafiti wetu. Nadharia ya Isimu Kongoo iliteuliwa kwani utafiti huu ulizingatia matatizo ya kitafsiri yanayotokana na kongoo inayotumika kama tafsiri ya maneno kwenye simu. Nadharia ya Tafsiri na haswa mtazamo wa

Nadharia ya Ulinganifu wa kimuundo imetumika kufidia upungufu wa dhana ya muundo wa maneno yanayotumika kama tafsiri kwa maneno, na ambao haujitokezi waziwazi katika Nadharia ya Isimu Kongoo. Pia, kongoo inatoa tu tafsiri bali haizingatii uwiano wa tafsiri iliyotolewa na muundo wa maneno ambayo yanaweza kuchukuliwa kuwa tafsiri bora. Nadharia hizi mbili zimefafanuliwa ili kudhihirisha jinsi ambavyo zimefidiana ili kutimiza malengo ya utafiti wetu.

### 1.8.1 Nadharia ya Isimu Kongoo

Kipengele cha lugha katika teknolojia ya simu na tarakilishi ndilo swala halisi ambalo limetafitiwa, hivyo utafiti huu ulitegemea lugha iliyohifadhiwa kikompyuta, ambayo haswa ndiyo kongoo. Nadharia au Mtazamo wa Kikongoo basi ilitumika katika uchanganuzi data wa utafiti huu kwa mujibu wa mihimili yake (Mahlberg, 2005).

Kwa mujibu wa Mahlberg (2005), sifa zinazobainisha nadharia hii ni kuwa lugha ni tukio la kijamii ambalo maana yake hujitokeza kwenye matumizi. Kamusi kwenye mtandao hutumia kongoo matini ambayo ni lugha halisi inayotumika kupitia kwa mbinu ya kielektroniki, na kwamba muundo na maana vina uhusiano kwa kuchunguza miundo anuai ya lugha inayoonekana katika kongoo.

Nadharia hii ilichukua nafasi kama nadharia kuu iliyoweza kuongoza utafiti huu. Ushahidi ni kuwa lugha hutoa maana yake kama tunavyoitumia kama wanajamii, kongoo iliyobuniwa haikuwa na maana pasi na kuhusishwa kwenye program za kikompyuta, na mwisho muundo na maana haviwezi kutenganishwa. Kwa upande mwingine kulikuwa na haja ya kuhusisha nadharia ya pili inayoweza kushughulikia swala la tafsiri kwani utafiti huu unaangazia maana ya maneno ambayo yanatolewa

kama tafsiri kwa maneno ya Kiingereza. Nadharia hii ya pili inafidia nadharia ya kwanza kwa kuwa ina vigezo vya kupimia lengo au malengo ya tafsiri katika kuwakilisha dhana ya maana ya neno.

### 1.8.2 Nadharia ya Tafsiri ya Ulinganifu wa Kimuundo

Nadharia ya Tafsiri hueleza kuhusu vipengele vinavyohusika katika kazi ya kutafsiri (Newmark 1982), nayo ina mihimili minne kuu ambayo ni Ulinganifu wa kimuundo, Usawe wa kidhima, Usawe wa aina-matini na Nadharia changamani. Utafiti huu ulihusisha Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo iliyoasisiwa na Cartford, (1969) ambapo utafiti huu uliangazia ubora wa miundo ya kongoo-matini inayotokea kama tafsiri kwa maneno ya Kiingereza.

Kwa mujibu wa Larson (1997), tafsiri ni sanaa na pia sayansi, kwani mtafsiri ananuia kufikia ufasaha wa matini asilia, kwa hivyo atatumia mbinu ya kisayansi ili kufanikisha usanii huo. Mtafsiri atatumia utaratibu mwafaka na wenye mantiki mbali na kuzingatia masharti kama vile muundo na maumbo ya maneno ambayo atayatoa hatimaye kama tafsiri mwafaka kwa maneno. Utaratibu huu humpa mtafsiri vigezo vya kuzingatia ili kuhakikisha mafanikio ya kazi ya tafsiri.

Hatua nne kuu za tafsiri ni uchambuzi wa matini ya lugha asili, uhamishaji wa maana ya kimsingi, uhawilishaji wa maana kulingana na lugha lengwa na usawidi wa matini ili kuhakikisha kuwa tafsiri imefanikiwa pasi na upungufu wowote. Nadharia iliyochunguza ufasaha wa tafsiri ni ile ya ulinganifu wa kimuundo ambao utafiti huu uliutumia kuchanganua data yake, pamoja na Nadharia ya Isimu Kongoo kwani matini inayochambuliwa ni kongoo kwenye simu na tarakilishi.

#### 1.8.2.1 Matumizi ya Nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo kwenye Utafiti

Katika utafiti huu, nadharia ya usawe wa kimuundo imetumika ili kuonyesha jinsi vile muundo wa maneno kwenye LC ya kongoo ambayo ni Kiingereza inavyopaswa kuwiana na muundo wa LL ya Kiswahili ili kutimiza malengo ya tafsiri. Tulizingatia ulinganifu wa maana kati ya maana halisi na maana potovu inayojitokeza kwenye tafsiri iliyotokana na muundo potovu wa maneno yaliyotafsiriwa. Kutokana na hali hii, viwango vyote vinne vya lugha vya sauti, silabi, neno na sentensi vitatumika ili kutathmini muundo wa maneno yaliyotolewa kama tafsiri na iwapo miundo hii inajitokeza kama tafsiri bora. Kwa vile nadharia ya Isimu Kongoo imejumuishwa

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Kwa mujibu wa Mugenda (2000), hakuna utafiti unaoweza kukamilika pasipo na matumizi ya mbinu za utafiti. Utafiti huu ni wa kitathmini kwa kuwa unakagua kongoo matini ya kamusi –tafsiri za mtandaoni na kutathmini ubora wake. Mbinu na ulinuia kutumia usampulishaji wa kimakusudi ili kuteua sampuli huku mbinu za maktaba na hojaji haswa zikitumika katika kukusanya data ambayo ilichanganuliwa baadaye.

### 1.9.1 Sampuli

Utafiti huu ni wa kitathmini na iliyotumia mbinu ya maelezo kwa wingi, na hivyo sampuli ya utafiti ilitokana na jumuiya ya watumizi mbalimbali wa kamusi za mtandaoni wakiwemo wanafunzo wa shahada ya uzamili wa chuo kikuu cha Kenyatta, wahadhiri mbalimbali, waandishi, na mtaalamu wa teknolojia.

Sampuli ni kiwakilishi cha idadi ya data ambayo mtafiti huzingatia katika utafiti wake kwa mujibu wa Gary (2009). Sampuli humsaidia mtafiti kupata matokeo bora

kuliko idadi yote kwa sababu ya uhaba wa muda na vifaa vya kufanyia utafiti mbali na kuepuka urudufu katika shughuli yake ya ukusanyaji. Uteuzi wa sampuli ni uchaguzi wa sehemu fulani ya watu au kitu ili kuwakilisha watu au kitu kizima Mugenda (1999). Sampuli ilipatikana kupitia uteuzi wa kimaksudi ambapo data ya kwanza ilitokana na maneno kialfabeti kwenye kamusi tafsiri za mtandao. Data ya pili ni ya watumizi mbalimbali wa kamusi za mtandaoni ambao ni watafitiwa wa utafiti wakiwemo walimu na wanafunzi wa shule za upili, wahadhiri na waandishi wa makala mbalimbali pamoja na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

#### 1.9.1.1 Uteuzi wa Sampuli

Jumuiya ya utafiti ilihusisha wahadhiri ambao ni waandishi wa vitabu na makala mbalimbali, wanafunzi wa shahada ya uzamili wa Kiswahili katika Chuo kikuu cha Kenyatta, walimu wa Idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya wavulana ya Kangundo na aghalabu mtaalamu wa maswala ya teknolojia. Watafitiwa hawa walitufaa zaidi katika utafiti kwani wana uwezekano wa kutumia kamusi za mtandao kwa wingi zaidi katika majukumu yao ya ufundishaji, usomi na uandishi wa makala mbalimbali na wana uwezekano mkubwa wa kuhitaji kupata tafsitri ya maneno ya Kiswahili.

Wahadhiri 5 wa Idara ya Kiswahili ya Chuo kikuu cha Kenyatta watateuliwa kimakusudi ili kusailiwa na kufanyiwa mahojiano na kupata data ya utafiti. Wahadhiri hawa walisaidia kupata data kuhusu tafsiri bora pamoja na matatizo ambayo huenda wamekumbana nayo katika harakati za ufundishaji na uandishi wa makala mbalimbali kwa wale ambao ni waandishi.

Walimu 7 wa idara ya Kiswahili katika shule ya upili ya Kangundo vile vile walihusishwa kupitia mahojiano na masaili ili kupata data ya ziada kuhusu utendakazi wa kamusi hizi. Mtafiti alihusisha wenzake 5 wa shahada ya uzamili wa Kiswahili katika utafiti pia, ikiwa ni 100% ya wanafunzi wa darasa hili katika mwaka huu. Kwa mujibu wa Krejcie na Morgan (1970), iwapo kuna idadi isiyozidi 10, basi wote wanafaa kufanyiwa utafiti. Watafitiwa hawa wote waliteuliwa kimakusudi na utafiti uliwalenga kwani ndio walio na uwezekano mkuu wa kuhitaji tafsiri kwa maneno ya Kiingereza.Idadi ya jumla ya utafiti huu ilikuwa watafitiwa 32, ilhali sampuli iliyozaliwa kwayo ilikuwa 18.

Mtafiti pia aliteua kimakusudi maneno ya Kiingereza kwenye kamusi za mtandaoni kuanzia alfabeti A na kutathmini tafsiri zao ili kubaini iwapo ni sahihi. Mtafiti alipitia kongoo ya maneno yaliyotafsiriwa hadi alfabeti M ili kuwa na habari za kutosha kutoa data. Kwa kadri, maneno kumi ya kila alfabeti yaliteuliwa na kufafanuliwa kulingana na aina zao kisha kubaini iwapo kuna tafsiri bora zaidi kwayo kwani aina ya neno huathiri tafsiri yake.

**Watu wote kwa Jumla**

Utafiti huu ulilenga watafitiwa 32 kwa jumla; wanafunzi wa shahada ya uzamili chuo kikuu cha Kenyatta mwaka 2020, wahadhiri 19, walimu wa Kiswahili 7, mtaalamu wa teknolojia 1 kama yanavyodhihirika katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 1.1: Watafiti wote Kwa Jumla**

| Watafitiwa | Watafiti wote kwa jumla | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Wanafunzi wa shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta mwaka 2020 | 6 | 18 |
| Wahadhiri | 19 | 58 |
| Walimu wa Kiswahili | 7 | 21 |
| Mtalaamu wa teknolojia | 1 | 3 |
| **Jumla** | **33** | **100** |

**Sampuli ya Utafiti**

Utafiti huu ulitumia sampuli ya wanafunzi wa shahada ya uzamili wa chuo kikuu cha Kenyatta mwaka 2020 6, wahadhiri 5, walimu wa Kiswahili 7 na mtaalamu wa teknolojia 1 kama yanavyodhihirika katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 1.2: Sampuli ya Utafiti**

| Watafitiwa | Sampuli | Asilimia % |
|---|---|---|
| Wanafunzi wa shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta mwaka 2020 | 6 | 32 |
| Wahadhiri | 5 | 26 |
| Walimu wa Kiswahili | 7 | 37 |
| Mtalaamu wa teknolojia | 1 | 5 |
| **Jumla** | **19** | **100 %** |

**Jedwali 1.3: Jinsi ya kupata Sampuli katika Jumuiya**

Jedwali hili linatoa mwongozo wa jinsi ya kupata sampuli katika jumuiya, na ni mwongozo uliotumika katika kupata sampuli ya utafiti huu.

| N | S | N | S | N | S |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | 10 | 220 | 140 | 1200 | 291 |
| 15 | 14 | 230 | 144 | 1300 | 297 |
| 20 | 19 | 240 | 148 | 1400 | 302 |
| 25 | 24 | 250 | 152 | 1500 | 306 |
| 30 | 28 | 260 | 155 | 1600 | 310 |
| 35 | 32 | 270 | 159 | 1700 | 313 |
| 40 | 36 | 280 | 162 | 1800 | 317 |
| 45 | 40 | 290 | 165 | 1900 | 320 |
| 50 | 44 | 300 | 169 | 2000 | 322 |
| 55 | 48 | 320 | 175 | 2200 | 327 |
| 60 | 52 | 340 | 181 | 2400 | 331 |
| 65 | 56 | 360 | 186 | 2600 | 335 |
| 70 | 59 | 380 | 191 | 2800 | 338 |
| 75 | 63 | 400 | 196 | 3000 | 341 |
| 80 | 66 | 420 | 201 | 3500 | 346 |
| 85 | 70 | 440 | 205 | 4000 | 351 |
| 90 | 73 | 460 | 210 | 4500 | 354 |
| 95 | 76 | 480 | 214 | 5000 | 357 |
| 100 | 80 | 500 | 217 | 6000 | 361 |
| 110 | 86 | 550 | 226 | 7000 | 364 |
| 120 | 92 | 600 | 234 | 8000 | 367 |
| 130 | 97 | 650 | 242 | 9000 | 368 |
| 140 | 103 | 700 | 248 | 10000 | 370 |
| 150 | 108 | 750 | 254 | 15000 | 375 |
| 160 | 113 | 800 | 260 | 20000 | 377 |
| 170 | 118 | 850 | 265 | 30000 | 379 |
| 180 | 123 | 900 | 269 | 40000 | 380 |
| 190 | 127 | 950 | 274 | 50000 | 381 |
| 200 | 132 | 1000 | 278 | 75000 | 382 |
| 210 | 136 | 1100 | 285 | 1000000 | 384 |

Note.—*N* is population size. *S* is sample size.

Source: Krejcie & Morgan, 1970

### 1.9.2 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data zilihusisha mbinu za usomaji maktabani, mahojiano na kujaza hojaji. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), matumizi ya mbinu zaidi ya moja una manufaa zaidi kuliko matumizi ya mbinu moja kwani huepusha upendeleo wa mtafiti. Vile vile mtafiti alikahikisha kuwa vigezo vya uhalali wa kimaudhiu na kimajibu umezingatiwa. Vigezo hivi

vilitumiwa ili kuhakikisha kuwa data inayokusanywa kwa kutumia kifaa fulani cha kukusanyia data hiyo kinaeleza ukweli kuhusu dhana inayofanyiwa utafiti.

#### 1.9.2.1 Mbinu ya Usomaji Maktaba

Mtafiti alinuia kutumia mbinu ya usomaji maktabani, ambapo alichukua muda mwingi kupitia tasnifu za awali zilizo na nakala zenye umuhimu na yanayohusiana na mada hii ya utafiti. Aliongozwa na maswali ya utafiti huu katika kuteua makala yaliyo na umuhimu katika machapishi ya awali, haswa makala yanayohusu teknolojia ya lugha pamoja na makala kuhusu uandishi wa kamusi.

#### 1.9.2.2 Hojaji

Hojaji ni maswali yaliyoandikwa ili data hiyo ikatumike katika kupata taarifa za utafiti (Mugenda, 1999). Mtafiti alitunga maswali yanayohusiana na utafiti wake ili kupata data anayohitaji kutoka kwa wahojiwa wake kupitia kwa majibu ya wahojiwa hawa. Wahojiwa hawa ni wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo cha Kenyatta, waandishi wa makala mbalimbali ya Kiswahili, wahadhiri wa Kiswahili pamoja na walimu wa Kiswahili wa shule ya upili ya Kangundo. Wahojiwa hawa walishirikishwa kwa kupewa nakala ya hojaji na kuhitajika kuyajibu maswali yaliyomo kwa ufasaha na kadri ya uwezo wao. Hojaji zetu zilihusisha maswali kwa watumizi mbalimbali wa kamusi teule za kitafsriri mtandaoni na jinsi walivyoathiriwa na tafsiri potovu kwenye kamusi hizi. Kamusi hizi ni zile za The English- Swahili Dictionary, English-Swahili offline Translator na English- Swahili Translator. Kisha hojaji zilikusanywa na kisha zikachanganuliwa.

#### 1.9.2.3 Mahojiano

Mahojiano ni mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi kuhusu mada fulani (Kothari, 2004). Mtafiti alitumia mwongozo wa mahojiano wenye maswali ili kupata habari kutoka kwa watafitiwa ili kufidia upungufi wowote utatakaoweza kutokea kutokana na matumizi ya hojaji. Maswali ya mahojiano yalioana na malengo ya utafiti ili kuhakikisha kuwa malengo hayo yameafikiwa.

### 1.9.3 Umuhimu na Utegemezi wa Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya kukusanya data (hojaji na masaili) vililainishwa hivi kwamba vilimwezesha mtafiti kupata habari inayostahili kutolewa kutokana navyo na kuambatana na malengo ya utafiti. Mbali na hayo, vyombo hivi vililainishwa (kwa kuwa na maswali yanayooana na mada ya utafiti) hivi kwamba viliweza kutoa habari ile ile inayotafitiwa kutoka kwa wasaili na wahojiwa tofauti tofauti. Mtafiti alizingatia haya katika kuandaa maswali ya mahojiano ili kumwezesha kutimiza lengo hili la kuwa na vifaa venye umuhimu na utegemezi wa kutosha katika utafiti wake.

### 1.9.4 Uchanganuzi wa Data

Data kutoka kwa kamusi ilichanganuliwa na kupangwa kialfabeti. Makosa ya kitafsiri yaliainishwa kuanzia maneno ya alfabeti 'A' hadi yale ya alfabeti 'M'. Mbali na hayo, data iliyopatikana kutokana na hojaji ilichanganuliwa ili kupata athari ya tafsiri isiyo sahihi kwa watumizi wa kamusi hizi. Katika uchanganuzi, tulitathmini kiini cha makosa haya, pamoja na athari ya makosa haya kwa watumizi wake, na njia zinazoweza kutumika kuboresha kamusi hizi. Uchanganuzi ulifanyika katika viwango vya maneno na sentensi, huku ukijikita haswa katika msamiati wa kawaida na wala si istilahi.

Ili kubaini makala yenye umuhimu, mtafiti aliongozwa na mihimili ya nadharia ya usawe wa kimuundo ili kuonyesha jinsi vile muundo wa maneno kwenye LC inavyopaswa kuwiana na muundo wa LL. Uchanganuzi ulihusisha ulinganifu wa maana kati ya maana halisi ya neno na maana potovu inayojitokeza kwenye kamusi-tafsiri za mtandaoni. Ulinganifu huu ulisababisha mtafiti kudondoa maneno ambayo aliyateua katika data yake.

### 1.9.5 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo na takwimu vile vile. Maelezo yalitolewa kwa ufupi huku yakiambatanishwa na majedwali kufafanua data kiasilimia ili kuhakikisha kuwa data hiyo ni ya kutegemewa.  Matokeo ya uchanganuzi wa maneno ambayo yametolewa kama tafsiri lakini yanapotosha yaliorodheshwa kialfabeti kwenye majedwali huku kukiwa na safu nyingine kutoa mapendekezo ya tafsiri bora kwa maneno hayo.

### 1.9.6 Maadili ya Utafiti

Mugenda na Mugenda (2012) wanaeleza kuwa ikiwa washiriki katika utafiti ni binadamu, sharti mtafiti aongozwe na maadili anapofanya utafiti. Utafiti huu ulizingatia maadili ya kiwango cha juu. Wahojiwa waliulizwa kama wangependa kushiriki katika kujibu maswali kwa hiari yao. Hakuna aliyeshurutishwa kutoa majibu katika hojaji au mahojiano. Vile vile, wahusika walihakikishiwa kuwa utambulisho wao utabakia kuwa wa faragha na kuwa taarifa zozote ambazo wangetoa zingetumiwa tu katika kufanikisha utafiti huu wala si kwa namna nyingine.

### 1.10 Hitimisho

Sura hii imetanguliza tasnifu hii kwa kutoa mwongozo na utaratibu wa utafiti. Sura hii imeshughulikia mada ya utafiti, suala linalotafitiwa pamoja na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii, upeo wa utafiti, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya kinadharia na mbinu za utafiti. Mtafiti alipambanua dhana hizi kwa tafsili na kimpangilio ili kufanikisha mfuatano wa kimantiki na kuelewa kwa makala. Maswala yaliyoshughulikiwa katika sura hii yamejenga msingi imara wa sura ya pili ambayo imeshughulikia lengo la kwanza la utafiti huu la kudondoa tafsiri potovu kwenye kamusi za mtandaoni.

# SURA YA PILI

# TAFSIRI POTOVU KATIKA KAMUSI TAFSIRI ZA MTANDAONI

## 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza ya utafiti huu, msingi wa utafiti umewekwa kwa kujadili usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya kinadharia na mbinu tulizotumia kukusanyia data ya utafiti huu. Katika sura hii ya pili, utafiti ulichanganua lengo la kwanza ambalo ni kubainisha tafsiri potovu katika kamusi za mtandaoni. Data zilizopatikana nyanjani kuhusu tafsiri potovu ya maneno katika kamusi-tafsiri za mtandaoni imechanganuliwa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya Isimu Kongoo (Mahlberg, 2005); lugha hutoa maana yake kama tunavyoitumia kama wanajamii.

Vile vile nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo (Newmark, 1982) imetumika; muundo wa maneno kwenye LC ya kongoo inapaswa kuwiana na muundo wa LL ili kutimiza malengo ya tafsiri. Maneno hayo yamepangwa katika alfabeti kutoka alfabeti A hadi alfabeti M kwa kutumia majedwali ambayo yameorodhesha mifano michache ya maneno ambayo yalitafsiriwa visivyo kwa kuzingatia alfabeti. Maneno ambayo yalikisiwa kuwa na tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni yamechanganuliwa na kuwekwa bayana.

## 2.1 Tafsiri Potovu katika Kamusi za Mtandaoni

Sehemu hii inaangazia data iliyochanganuliwa ili kubainisha tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Uchangunizi huu umeongozwa na misingi ya nadharia ya tafsiri ya ulinganifu wa kimundo ambayo ni nadharia iliyotumika kuchanganua data.

### 2.1.1Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti A

Mtafiti aliweza kuchanganua baadhi ya maneno kwenye alfabeti ya A ili kutathmini tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni kisha kuwasilisha data hii. Jedwali 2.1. linaonyesha maneno haya na yalidondolewa katika kamusi ya the English – Swahili Offline Translator.

**Jedwali 2.1: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti A**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Abduct | Kuwateka | Teka |
| Abort | Mimba | Avya |
| Aborted | Kwa hiari | Aliavya |
| Admiral | Penda | Yenye kupendeka |
| Adulthood | Watu wazima | Utu uzima |
| Advise | Ushauri | Shauri |
| African | Afrika | Mwafrika |
| Agreeable | Mazuri | Kukubalika |
| America | Amerika ya | Amerika |


Jedwali 2.1 linaonyesha tafsiri potovu ikilinganishwa na tafsiri bora kwa kuzingatia vigezo mbali mbali. Kwa mfano, kwa kuzingatia kigezo cha Usawe wa Kimuundo, neno la Kiingereza ‘Abduct’ limetafsiriwa kama kuwateka katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni badala ya teka. Kuongeza viambishi *ku-* na *wa-* katika neno teka kunabadilisha maana ya neno hilo kimsingi. Tafsiri sawia ya neno kuwateka katika lugha ya Kiingereza ni ‘abducting them’. Neno ‘abort’ limetafsiriwa kama mimba badala ya avya. Kwa kurejelea kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI toleo la nne, maana ya msingi ya neno mimba ni kiumbe ambaye hajazaliwa tofauti na neno la

Kiingereza ‘abort’ ambalo tafsiri yake katika Kiswahili ni avya tofauti na jinsi limetafsiriwa katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni.

Kwa upande mwingine, neno ‘abort’ ni kitenzi ilhali neno mimba ni nomino, kinyume na mhimili wa nadharia ya Ulingafu wa Kimuundo kuwa muundo wa neno kwenye LC ya kongoo inapaswa kuwiana na muundo wa LL ili kutimiza lengo la tafsiri. Mfano huu pia unaonyesha makosa ya uhawilishaji wa maana katika lugha lengwa. Kulingana na Jilala (2014), katika kuhawilisha maana, sharti ulinganifu wa visawe vya LC na LL uzingatiwe kikamilifu.

**Kielelezo 2.1: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti A katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni**

Kielelezo 2.1 ni taswira halisi ya jinsi vile kamusi-tafsiri ya mtandao, aina ya *English-Swahili online Translator* ilivyotoa ya neno ‘Awake’, lenye tafsiri kuwa macho wala si ‘macho’ ambalo tafsiri yake kwa kuzingatia maana ya kimsingi ni ‘eyes’. Isipokuwa katika muktadha wa sentensi huenda neno hilo likatumika kama kuwa macho, kutumia neno macho moja kwa moja kama tafsiri kwa neno hilo kunaleta upotovu wa tasiri.



### 2.1.2 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti B

Mtafiti alichagua baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri za mtandaoni na kuzichanganua ilikubainisha tafsiri potovu katika tafsiri ya maneno hayo. Jedwali 2.2 linadokeza baadhi ya maneno yaliyochanganuliwa kwenye alfabeti B. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Translator.

**Jedwali2.2: Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti B**


| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Ball | Cheza | Mpira |
| Beehives | Dependence | Mizinga |
| Bitter | Uchungu | Chungu |
| Bleed | Elbow | Vuja |
| Block | Inafanya | Zuia |
| Boil | Waoga | Tokota/jipu |
| Breast | Msamaha | Titi |
| Breathe | Maonyesho | Pumua |
| Brick | Matofali | Tofali |

Kutokana na Jedwali 2.2, maneno haya yamepewa tafsiri ambayo huenda inahusiana na neno lenyewe wala si tafsiri sahihi ama tafsiri ambayo haina uhusiano kabisa na neno lenyewe.  Kwa mfano, tafsiri ya neno ‘Ball’ katika kamusi ya TUKI ni mpira lakini katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni neno hilo limetafsiriwa kama nacheza neno ambalo linatafsiriwa katika Kiingereza kama ‘play’. Kwa upande mwingine, neno ‘Breathe’ halina uhusiano wowote na neno maonyesho ambalo limetolewa kama tafsiri yake ya kimsingi. Neno ‘Bleed’ limetafsiriwa kama ‘elbows’ neno ambalo ni la Kiingereza lililo na maana tofauti isiyohusiana na neno linalotafsiriwa kinyume na mhimili wa nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo kuwa maana jinsi ilivyokusudiwa katika lugha chanzi sharti ilingane na maana katika lugha lengwa.

Vilevile, mifano sawia kwenye Jedwali 2.2 inaonyesha maneno yaliyotafsiriwa visivyo kwa kutofuata kanuni za kutafsiri. Kaviti (2005) anasisitiza kuwa katika tafsiri, kuna umuhimu wa kusawazisha sintaksia ndipo maana ya ujumbe asilia imfikie msomaji.

**Kielelezo2.2: Tafsiri Potovu Ya Neno 'Busy' Kwenye Alfabeti B Katika Kamusi-Tafsiri Ya Mtandaoni**

Kielelezo 2.2 kinaonyesha tafsiri ya neno 'Busy' ambalo halijapewa tafsiri yoyote ile bali limebakia kuwa jinsi lilivyo.




### 2.1.3 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti C

Mtafiti alichanganua tafsiri ya baadhi ya maneno katika kamusi-tafsiri za mtandaoni kwenye alfabeti ya C ili kubaini kama baadhi ya maneno hayo yana tafsiri potovu. Jedwali 2.3 linaonyesha data iliyochanganuliwa kwenye alfabeti C. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Offline Translator.

**Jedwali 2.3: Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti C**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Coach | Isiyokuwa | Kocha |
| Church advocate | Kanisa wakili | Wakili wa kanisa |
| Chase | Baada | Fukuza |
| Choking | Nenda | Kunyonga |
| Chicken heart | Kuku moyo | Moyo wa kuku |
| Claim | Madai | Dai |
| Class | Darasani | Darasa |
| Chlamydia | Kahaba | Klamidia (ugonjwa) |
| Chameleon | | Kinyonga |

Jedwali 2.3 linaorodhesha data ya baadhi ya maneno kwenye alfabeti C ambayo hayana tafsiri bora katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Katika tafsiri ya baadhi ya maneno katika alfabeti ya C, tofauti ya kimuundo kati ya Kiswahili na Kiingereza inaonekana kuleta tatizo. Kwa mfano kifungu cha maneno 'Church advocate' limetafsiriwa kama kanisa wakili. Tafsiri hii ni ya moja kwa moja na hivyo inakosa kuleta maana iliyokusudiwa katika LL kwa sababu lugha hizi mbili zinatofautiana kimuundo. Kifungu kingine ni 'Chicken heart' ambacho kimetafsiriwa moja kwa moja kama kuku moyo. Mfano mwingine ni neno kama vile 'Class' ambalo limetafsiriwa kama darasani na kuleta dhana ya kielezi cha mahali badala ya nomino darasa. Katika mfano huu, kanuni za kisarufi zimekosa kuzingatiwa. Iwapo neno la Kiingereza ni nomino, ni jambo la muhimu sana kuwa tafsiri yake pia iwe nomino wala sio aina nyingine ya neno (Jilala, 2014). Kulingana na nadharia ya Usawe wa

Kimuundo, muundo wa maneno kwenye lugha chanzi unapaswa kuwiana na muundo wa lugha lengwa ili kutimiza malengo ya tafsiri.

### 2.1.4 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti D

Mtafiti alidadisi baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri za mtandaoni kwenye alfabeti ya D ili kubaini kama kulikuwa na tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 2.4 linaonyesha tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti D. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Translator.


**Jedwali 2.4: Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti D**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Drive | Kutekwa | Endesha |
| Deaconhood | Shemasi kofia | Ushemasi |
| Delete | Kufuta | Futa |
| Ditch | Shimoni | Mtaro |
| Dribbling | Dribbling | Pepeta |
| Drinkable | Hutamkwa | Nyweka |
| Drinker | Mlevi | Mnywaji |
| Disease | Magonjwa | Ugonjwa |
| Dear | Wapenzi | Mpendwa |
| | | |

Kwenye jedwali 2.4,inadhihirika kuwa maneno mengi yametafsiriwa visivyo. Kwa mfano, inaonekana kuwa neno ‘Drive’ lenye maana endesha kama vile gari limetafsiriwa kama kutekwa. Neno ‘Drive’ halipo katika muktadha wa sentensi na hivyo maana iliyosudiwa kutolewa ni ile ya kimsingi. Pia, neno ‘Drinker’ limetafsiriwa kama mlevi badala ya mnywaji, kwani tafsiri ya Kiingereza ya neno mlevi ni ‘Drunkard’. Neno ‘Disease’ liko katika hali ya umoja lakini tafsiri yake imetolewa katika hali ya wingi na hivyo kufanya tafsiri ya neno hilo kupotoka. Neno ‘Drinkable’ lina maana ya kuwa kitu kiowevu kinanyweka wala si ‘Hutamkwa’

kama ilivyopachikwa kwenye kamusi hii. Neno ‘Dribbling’ halijatafsiriwa bali limebakia kuwa vile vile. Kutokana na mifano hii, suala jingine linalojitokeza ni kuwa lazima hali ya nomino katika Kiingereza izingatie tafsiri ya Kiswahili inapotolewa kwenye kamusi hizi. Pia, aina ya neno sharti izingatiwe hivi kwamba kama neno ni kielezi, basi tafsiri itolewe kama kielezi wala si kama kivumishi (Jilala, 2014). Katika muktadha huu, mhimili wa nadharia ya Ulingafu wa Kimuundo kuwa muundo wa maneno kwenye LC ya kongoo ambayo ni ya Kiingereza yanapaswa kuwiana na muundo wa LL ya Kiswahili ili kutimiza malengo ya tafsiri haujazingatiwa.

**Kielelezo 2.3-kina mfano wa tafsiri potovu ya neno ‘Drive’ kwenye alfabeti D katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni**




### 2.1.5 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti E

Mtafiti alichunguza baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri za mtandaoni kwenye alfabeti ya E ili kubaini kama kulikuwa na tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 2.5 linaonyesha data iliyochanganuliwa kwenye alfabeti E. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Dictionary.


**Jedwali 2.5: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti E**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Ear | Nyekundu | Sikio |
| Eighteenth | Kumi na nane | -a kumi na nane |
| Enabler | Kufikiria | Mwenye kuwezesha |
| Enormously | Nyoka | Kikubwa |
| Envying | Wivu | Kuonea wivu |
| Errand | Kafara | Matembezi |
| Etc | Sakramenti | Na kadhalika |

Katika Jedwali 2.5, maneno mengi yametafsiriwa visivyo. Kwa mfano, neno ‘English’ ambalo maana yake ya kimsingi ni Kiingereza limetafsiriwa kama anajibu. Hata kama neno anajibu lingekuwa sahihi, bado neno hilo si nomino ikizingatiwa kuwa neno ‘English’ ambalo linarejelewa ni nomino huku neno anajibu likiwa kitenzi. Vilevile, neno ‘Ear’ limetafsiriwa kama nyekundu badala ya sikio, ikizingatiwa kuwa tafsiri ya Kiingereza ya neno sikio ni ‘Ear’. Neno ‘Entertain’ lina maana ya tumbuiza wala si ‘Kuwakaribisha’ kama ilivyodokezwa kwenye kamusi tafsiri. Kutokana na mifano hii, inajitokeza kuwa maneno mengine yametafsiriwa kwa kutozingatia maana ya kimsingi ya LC na kuioanisha na ile ya LL. Kaviti (2005) anaelezea kuwa katika tafsiri, kuna haja ya kusawazisha sitanksia ili ujumbe asilia umfikie msomaji. Katika mifano ambayo tumeangazia, kanuni ya kusawazisha sitanksia inaonekana kupuuzilia na hivyo basi matokeo yake kuwa tafsiri potovu.

**Kielelezo 2.4: Tafsiri Potovu ya Neno 'envying' kwenye Alfabeti E katika Kamusi-tafsiri ya Mtandaoni**

Kielelezo 2.4 kinaonyesha mfano wa tafsiri wa neno 'envying' kwenye alfabeti E lililotafsiriwa kama wivu katika Kiswahili badala ya kuonea wivu.




### 2.1.6 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti F

Mtafiti alichunguza baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kwenye alfabeti ya F ili kubaini kama kulikuwa na tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 3.6 linaorodheshamifano ya maneno yaliyotafitiwa kwenye alfabeti F. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Offline Translator.

**Jedwali 2.6: Tafsiri Potovu ya Maneno kwenye Alfabeti F**


| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Fall | Kuanguka | Anguka |
| Fiances | Fiancés | Wachumba |
| Fig | Mitini | Zabibu |
| Fin | Mwisho | Mbawa wa samaki |
| Fighter pilot | Majaribio fighter | Rubani mpiganaji |

| | | |
|---|---|---|
| Fishbone | Samaki mfupa | Mfupa wa samaki |
| Flow | Kati yake | Tiririka |

Katika Jedwali 2.6, inadhihirika kuwa maneno mengi yalitarfsiriwa visivyo kwani tafsiri yazo inabadilisha aina ya maneno mbali na kuwa na athari ya tafsiri sisisi. Neno kama vile 'Fish bone' limetafsiriwa kama samaki mfupa kwa namna ya tafsiri sisisi, na hivyo kuharibu tafsiri ya neno hilo kwani haliwezi kutumika hivyo katika usemi wala maandishi kwani neno 'bone' linatumika kumaanisha mfupa wa samaki wala si neno moja (samaki-mfupa). Nenon'Fig' limetafsiriwa kama mitini. Kwa kurejelea uhamishaji wa maana ya kimsingi ya neno katika hatua za kutafsiri, maana ya kimsingi ya neno 'Fig' ni zabibu wala si mitini jinsi lilivyotafsiriwa katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni. Shitemi (1990) anaeleza kuwa matini ya lugha chanzi na lugha pokezi yanaweza kutofautiana kwa sababu za uteuzi kwa ajili ya kuwasilisha ujumbe kwa njia bora zaidi wala si kimakosa.

**Kielelezo 2.5: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti F katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni**

Kielelezo 2.5 kinaonyesha tafsiri ya neno 'fin' katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni ambalo limetafsiriwa kama mwisho katika Kiswahili, badala ya mbawa wa samaki.



### 2.1.7 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti G

Mtafiti alichunguza baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kwenye alfabeti ya G ili kubaini kama kulikuwa na tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 2.7 linaonyesha data baada ya uchunzaji kwenye alfabeti G. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Translator.

**Jedwali 2.7: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti G**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Giant killer | Kubwa muuaji | Muuaji mkubwa |
| Giant lizard | Kubwa mjusi | Mjusi mkubwa |
| Glow | Mwanga | Ng'aa |
| Good | Bora | Nzuri |
| Grades | Darasa | Daraja |
| Grab | Kunyakua | Nyakua |
| Groan | Tunaugua | Ugua |

Kwa kuzingatia Jedwali 2.7, neno 'Giant killer' limetafsiriwa kama kubwa muuwaji badala ya muuwaji mkubwa, na kukiuka sheria ya kisarufi ambapo kivumishi hakiwezi kuitangulia nomino katika lugha ya Kiswahili. Vilevile, neno 'Glow' linamaanisha ng'aa wala si mwanga ambalo kisawe chake ni nuru.Kulinganana mifano iliyojitokeza katika Jedwali 2.7, suala la ukiukaji wa sheria za kisarufi katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni linajitokeza. Vile vile, suala la tofauti za kimtindo kati ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili linajitokeza mathalani katika neno 'Giant lizard' ambalo limetafsiriwa moja kwa moja kama kubwa mjusi badala ya mjusi mkubwa. Katika mfano huu, kivumishi kimetangulia nomino badala ya nomino

kuitangulia kivumishi jinsi mpangilio wa maneno ulivyo katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Larson (1997), mtafsiri anahitajika kutumia utaratibu mwafaka na wenye mantiki mbali na kuzingatia masharti kama vile muundo na maumbo ya maneno ambayo atayatoa hatimaye kama tafsiri mwafaka kwa maneno.

**Kielelezo 2.6: Tafsiri Potovu Cha neno 'glow' kwenye Alfabeti G Katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni ambayo imetafsiriwa kama Mwanga katika Kiswahili.**




### 2.1.8 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti H

Mtafiti alichunguza baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kwenye alfabeti ya H ili kubaini kama kulikuwa na tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 2.8 linaweka bayana data iliyochanganuliwa kwenye alfabeti H. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Dictionary.


**Jedwali 2.8: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti H**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Habit | Zoezi | Mazoea |
| Head back | Kichwa nyuma | Nyuma ya kichwa |
| Heavenly | Mbinguni | Kimbinguni |
| Heifer | Ng'ombe | Ndama |
| Hold | Shikashikilia | Shikilia |
| Horizon | Usawa | Upeo wa macho |
| Humiliate | Kudhalilisha | Dhalilisha |
| | | |

Katika Jedwali 2.8 neno ‘Humiliate’ lina maana ya kudhalilisha au kushusha mtu hadhi, ambalo ni kitenzi, hata hivyo kuambisha neno hilo katika Kiswahili kunaleta dhana ya nomino, na basi tafsiri bora ni ‘dhalilisha’ pasi na kuongeza kiambishi. Jambo jingine ni kuwa, vivumishi lazima vitafsiriwe kama vivumishi wala si kufanywa nomino ama aina nyingine ya neno, kama vile ‘Heavenly’ si Mbinguni bali ni kimbinguni. Katika mifano hii, kanuni za kisarufi zimekiukwa. Kwa mujibu wa Jilala (2014), tafsiri bora sharti izingatie kanuni zote za kisarufi. Aidha, kwa mujibu wa nadharia ya Usawe wa Kimuundo, muundo wa maneno katika LC unafaa kuwiana na ule wa LL. Sharti hili limekiukwa katika mfano wa maneno ‘Head back’ ambapo maneno hayo yametafsiriwa kwa kuzingatia muundo wa Kiingereza badala ya kuhakikisha kuwa kuna uwiano wa miundo katika tafsiri.

**Kielelezo 2.7: Tafsiri Potovu Cha neno ‘humiliate’ kwenye Alfabeti H Katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni**

Kielelezo 2.7 kinaonyesha tafsiri ya neno ‘humiliate’ katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni ambapo neno hilo limetafsiriwa kama kudhalilisha.




### 2.1.9 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti J

Utafiti ulichunguza baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kwenye alfabeti ya J ili kufahamu kama kulikuwa na tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 2.9 linaweka bayana data iliyochanganuliwa kwenye alfabeti J. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Offline Translator.


**Jedwali 2.9: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti J**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Jackal | Jackal | Mbweha |
| Jail | Korokoroni | Gereza/jela |
| Job | Testi | Kazi |
| Joke | Furaha | Utani/mzaha |
| Joyful | Furaha | -enye furaha |
| Joiner | Seremala | Anayejiunga |
| Juggle | Juggle | Jongea |

Katika Jedwali 2.9, kwenye alfabeti J, neno kama vile 'Jackal' halijatafsiriwa kwani tafsiri yake ni mbweha. Badala yake, neno hilo limeandikwa tu kama 'Jackal' kumaanishwa kuwa tafsiri yake ilibakia kuwa vile vile. Katika mfano huu, mtumiaji wa kamusi-tafsiri hii ya English – Swahili Offline Translator anaweza kulichulia neno 'Jackal' kama neno la Kiswahili kwa sababu hivyo ndivyo limetafsiriwa. Kwa mujibu wa Jilala (2014), katika tafsiri, mfasiri sharti azingatie ulinganifu wa visawe vya LC na LL sharti ambalo linaonekana kupuuzwa katika mfano huu. Pia, neno 'Joyful' ni kivumishi ambacho tafsiri yake ni –enye furaha wala sio nomimo furaha.

**Kielelezo 2.8: Tafsiri Potovu Cha neno 'humiliate' kwenye Alfabeti J Katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni**

Kielelezo 2.8 kinaonyesha tafsiri ya neno 'juggle' katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni ambapo neno hilo limeandikwa tu katika Kiswahili kama 'juggle' badala ya jongea.




### 2.1.10 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti L

Utafiti ulichunguza baadhi ya tafsiri za maneno katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kwenye alfabeti ya L ili kubainisha tafsiri potovu katika maneno hayo. Jedwali 3.10 linaweka bayana data iliyochanguliwa kwenye alfabeti L. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Translator.


**Jedwali 2.10: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti L**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Label | Studio | Lebo |
| Liability | Dhima | Deni |
| Leave | Shika | Ondoka |
| Long | Muda mrefu | Ndefu |
| Lazy | Uvivu | Mvivu/wavivu |
| Look | Pendeza | Tazama |
| Lack | Fahari | Ukosekanaji |
| Load bearing | Mzigo kuzaa | Kubeba mzigo |
| Lown | Chini | Bustani la maua |

Katika Jedwali 2.10, kwenye alfabeti L, neno 'Leave' limeafsiriwa visivyo kwani tafsiri yake niondoka wala si shika. Neno 'Lack' limetafsiriwa kama fahari badala ya ukosekanaji. Mifano hii miwili inaonyesha kukosekana kwa ulinganifu wa maana na ujumbe wa visawe vya LC na LL. Kwa mujibu wa Shitemi (1990), katika tafsiri, ulinganifu wa maana na ujumbe wa LC na LL sharti uzingatiwe. Mfano mwingine ni neno 'Load bearing' ambalo tafsiri yake ni kubeba mzigo wala sio 'Mzigo kuzaa' vile lilivyotafsiriwa katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni. Vile vile, neno 'mzigo kuzaa' limeborongwa na halifuati kanuni ya kisarufi katika lugha Kiswahili.

**Kielelezo 2.9: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti L katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni**

Kielelezo 2.9 kinaonyesho tafsiri ya neno 'lown' katika kamusi tafsiri-ya mtandaoni ambapo neno hilo limetafsiriwa kama katika Kiswahili kama chini.




### 2.1.11 Tafsiri Potovu ya Maneno Chini ya Alfabeti M

Mtafiti alidadisi baadhi ya tafsiri ya maneno katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kwenye alfabeti ya M ili kubainisha tafsiri potovu katika maneno hayo jinsi ilivyoonyeshwa katika Jedwali 2.11. Maneno haya yalidondolewa katika kamusi ya The English – Swahili Offline Translator.

**Jedwali 2.11: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti M**

| NENO LA KIINGEREZA | TAFSIRI POTOVU | TAFSIRI BORA |
|---|---|---|
| Minute book | Dakika ya kitabu | Kitabu cha kumbukumbu |
| Misadvise | Misadvise | Kutoa ushauri potovu |
| Mum | Mum | Mama |
| Mimba | Abort | Ujauzito |
| Mouth | Musings | Mdomo |
| Millionaire | Millionary | Milionea |
| Mingling | Minglingly | Tangamana |
| Move | Hoja | Songa |

Katika Jedwali 2.11, neno 'Mum' ambalo maana yake ya kimsingi ni mama halijatafsiriwa bali limebaki vile vile. Neno 'Moist' ambalo tafsiri yake ya kimsingi

ni unyevunyevu limetafsiriwa kama baridi, nalo neno ‘Mouth’ ambalo tafsiri yake ya kimsingi ni mdomo limetafsiriwa kama ‘Musings’. Katika mifano hii ambayo tumeiangazia, maana ya kimsingi ya maneno haijajitokeza katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni. Larson (1997) akirejelea nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo anaangazia hatua nne kuu za tafsiri ambazo ni uchambuzi wa matini ya lugha asili, uhamishaji wa maana ya kimsingi, uhawilishaja wa maana kulingana na lugha lengwa na usawidi wa matini ili kuhakikisha kuwa tafsiri imefanikiwa pasi na upungufu wowote.

**Kielelezo 2.10: Tafsiri potovu ya maneno kwenye alfabeti M katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni**

Kielelezo 2.10 kinaonyesha tafsiri ya neno ‘move’ katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni ambapo neno hilo limetafsiriwa katika Kiswahili kama hoja.




## 2.2 HITIMISHO

Kwa mujibu wa malengo ya utafiti wetu, mtafiti aliweza kukusanya data hii kwa kuzingatia mipaka ya alfabeti A- M. Aliweza kuchunguza na kudondoa maneno ambayo yalikuwa na tafsiri isiyofaa na kutoa mapendekezo ya tafsiri ambayo inaweza kuwa bora zaidi kuliko maneno yaliyotolewa kwenye kamusi hizi. Hili

limefanywa kupitia mifano ya maneno yaliyotolewa kwenye majedwali na michoro. Kila jedwali lilikuwa na safu tatu ambapo safu ya kwanza ilikuwa na maneno ya Kiingereza, safu ya pili ilikuwa na tafsiri potovu ya maneno nayo safu ya tatu ilitoa mapendekezo ya tafsiri bora zaidi kuliko ile iliyotolewa kwenye kamusi hizi kwa mujibu wa mapendekezo ya wataalamu wa lugha pamoja na kuangazia kamusi na vitabu vingine vilivyochapishwa.

Mifano iliyotolewa kwenye kila alfaeti iliweza kuonyesha namna upotovu katika tafsiri ilivyodhihirika. Baadhi ya tafsiri ilitumia maneno yenye ukuruba na tafsiri mwafaka kwa kutumia vigezo vya kinadharia badala ya kutumia tafsiri mahususi. Baadhi ya maneno yalikuwa na maana tofauti kabisa kwa kuzingatia aina ya maneno yake ya Kiingereza na mwisho baadhi ya tafsiri ilikuwa na maneno ambayo hayana uhusiano wowote na maneno ya LL, na hivyo kukawa na tafsiri isiyoweza kukubalika. Jambo la muhimu lililotokana na utafiti huu ni kwamba kuna haja ya kamusi hizi kupigwa msasa ili wanaozitegemea wakanfaike zaidi. Pia, kutasaidia haswa wale wanaofanya kazi ya lutafsiri vitabu na makala mbali mbali kwa kutegemea kamusi- tafsiri za mtandaoni.  Katika sura ya tatu, utafiti umeangazia vyanzo vya tafsiri hii tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni.

# SURA YA TATU

# VYANZO VYA TAFSIRI POTOVU KATIKA KAMUSI TAFSIRI ZA MTANDAONI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili iliyotangulia, utafiti huu umechunguza tafsiri potovu katika kamusi za mtandaoni ambapo ilibainika kuwa tafsiri ya baadhi ya maneno katika kamusi za mtandaoni ni potovu. Makosa haya yalihusiana na mwendelezo wa maneno ama matumizi ya kongoo isiyofaa na hivyo kupoteza maana ya neno-tafsiri ama neno lake la Kiingereza. Sura hii ya tatu ilichunguza vyanzo vya tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni kwa misingi wa mihimili ya nadharia mbili zinazoongoza utafiti huu ambazo ni nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo na Nadharia ya Isimu Kongoo kwa kuzingatia vigezo vya kiisimu vya mofolojia, sintaksia na pragmatiki.

## 3.1 Vyanzo vya Tafsiri Potovu katika Kamusi Tafsiri za Mtandaoni

Katika sura hii, uchanganuzi wa data ulilenga kubaini vyanzo vya makosa katika kamusi tafsiri za mtandaoni. Baadhi ya vyanzo vya tafsiri potovu ambavyo vimechanganuliwa ni pamoja na: Tofauti za muundo wa lugha, tofauti za kimtindo kati ya lugha, matatizo ya uteuzi wa msamiati, udurusu wa kongoo-matini kupuuzwa au kufanyika kiholela, kutokuwepo kwa sera za kuhakikisha uboreshaji wa kamusi-tafsiri za mtandaoni mara kwa mara, kutokuwa kwa sera ya kuhakiki na kusawazisha kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao, upana wa maneno na kuzuka kwa misamiati ya Kiingereza na Kiswahili, swala la lugha ya Kiswahili kukua, makosa ya kiufundi; kukagua tahajia, na makosa kutokana na hali/ mambo mengineyo. Vile vile, vyanzo vingine vilivyochanganuliwa ni mambo ambayo

hujitokeza katika viwango anuwai vya makosa vinavyoathiri ubora wa tafsiri kama vile makosa katika kiwango cha mofolojia, makosa katika kiwango cha semantiki, na makosa katika kiwango cha pragmatiki. Kulingana na mada ya utafiti, mapendekezo yameweza kutolewa kwa baadhi ya maneno ambayo yanayoonelewa kuwa bora zaidi kwa tafsiri ya maneno. Data hii ilitokana na vyombo vya utafiti vya mahojiano, masaili na utafiti wa maktabani.

### 3.1.1 Tofauti za Muundo wa Lugha ya Kiswahili na Muundo wa Lugha ya Kiingereza

Kulingana na Jilala (2014), muundo wa lugha una viwango vinne ambavyo ni grafolojia, fonolojia, leksia na sarufi. Viwango vya leksia na sarufi vinachukua umuhimu zaidi katika sehemu hii kwani tafsiri nyingi huzingatia leksia za maneno na kanuni za kisarufi. Jedwali 3.1 linaonyesha tofauti za muundo wa lugha ya Kiswahili na muundo wa lugha ya Kiingereza.

**Jedwali 3.1: Tofauti Za Muundo Wa Lugha Ya Kiswahili Na Muundo Wa Lugha Ya Kiingereza**

| Neno la Kiingereza | Tafsiri katika kamusi-tafsiri za mtandaoni | Tafsiri bora |
|---|---|---|
| Arm na Hand | Mkono | Mkono |
| History book | Historia kitabu | Kitabu cha Historia |
| Giant lizard | Kubwa mjusi | Jusi |

(Mifano hii imetoka kwa The English- Swahili Online Translator)

Katika Jedwali 3.1 Leksia za Kiingereza **'arm'** ama **'hand'**zimetafsiriwa kijumla katika Kiswahili kama 'mkono'.Katika kiwango cha leksia, maana ya msingi ya neno huangaziwa na maana hii inafaa kujitokeza katika tafsiri ya neno (Jilala, 2014). Hata hivyo, lugha ya Kiingereza inaweza kuwa na leksia mbili kwa neno ambalo lina leksia moja katika Kiswahili na hivyo kuleta utata wakati wa tafsiri haswa iwapo neno ambalo linapatikana kwa Kiswahili likionekana kuwa la mbali kama tafsiri. Mfano wa pili ni ule ambao lugha ya Kiingereza huanza kwa kivumishi kisha nomino tofauti na lugha ya Kiswahili ambayo kivumishi hufuata nomino vile inavyojitokeza katika Jedwali 3.1 kwenye neno 'History book' linalotafsiriwa kama Historia Kitabu, na 'Giant lizard' kutafsiriwa kama Kubwa mjusi. Kwa hivyo, baadhi ya maneno yanatafsiriwa visivyo pale ambapo kanuni ya Kiingereza zinatumika badala ya ile ya Kiswahili katika kutafsiri. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo, muundo wa maneno kwenye LC ya kongoo ambayo ni Kiingereza inapaswa kuwiana na muundo wa LL ya Kiswahili ili kutimiza malengo ya tafsiri.

### 3.1.2 Tofauti za Kimitindo Kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza

Mitindo, au sajili za lugha ni matumizi ya lugha katika muktadha maalum (Mgullu, 1999). Jedwali 3.2 linaonyesha tofauti za kimtindo kati ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**Jedwali 3.2: Tofauti Za Kimtindo Kati Ya Lugha Ya Kiswahili Na Kiingereza**

| **Neno la Kiingereza** | **Tafsiri katika kamusi-tafsiri za mtandaoni** | **Tafsiri bora** |
|---|---|---|
| Thou shall not steal (mtindo wa kidini) | Usiibe/Msiibe | Usiibe(iwapo mrejelewa ni mmoja na msiibe iwapo ni zaidi ya moja |
| Do not steal (mtindo wa kawaida) | Usiibe/Msiibe | Usiibe(iwapo mrejelewa ni mmoja na msiibe iwapo ni zaidi ya moja |

(Mabeya, 2012)

Jedwali 3.2 linadhihirisha tofauti za kimtindo kati ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Maneno ya mtindo wa kidini katika lugha ya Kiingereza 'Thou shall not steal' ambayo mtindo wake wa kawaida ni 'do not steal' yanatafsiriwa kwa Kiswahili kwa muktadha wa kawaida 'usiibe'. Mwangi (2016) anafafanua kuwa katika tafsiri ya wingi-lugha, mitindo ya lugha inaweza kuleta vikwazo katika tafsiri. Katika mfano ulio katika Jedwali 3.2, tunaona kuwa mitindo mbalimbali ya lugha hufanikisha mawasiliano katika muktadha maalum, na wala sio katika muktadha wowote. Hivyo basi, imejitokeza kuwa tafsiri ya maneno katika muktadha maalum inaweza kuwa na matatizo iwapo itatumika katika muktadha mwingine. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo, maana jinsi ilivyokusudiwa katika lugha chanzi sharti ilingane na maana katika lugha lengwa.

### 3.1.3 Matatizo Ya Uteuzi Wa Msamiati/Maneno Maalum

Ni vigumu kupata maana kamili ya maneno ambayo yamekita katika utamaduni wa LC ambayo hayana tafsiri sahihi katika LL. Jedwali 3.3 linaonyesha matatizo ya uteuzi wa msamiati/maneno maalum.

**Jedwali 3.3: Matatizo Ya Uteuzi Wa Msamiati/Maneno Maalum**

| **Neno la Kiingereza** | **Tafsiri katika Kamusi ya mtandaoni** | **Tafsiri bora** |
|---|---|---|
| Drinking basket/ Bucket | Ndoo | Ndoo ya kunywia / ndoo |
| Ice skating | Ice skating | Kuteleza barafuni |
| High Tea | High Tea | - Halina tafsiri |

Katika Jedwali 3.3, maneno ya Kiingereza 'Drinking basket/bucket' yametafsiriwa kwa neno moja kama ndoo katika Kiswahili. 'Drinking basket' ni msamiati wa kitamaduni katika lugha ya Kiingereza ambao hauna tafsiri sambamba katika Kiswahili. Maneno 'Ice skating' na 'High tea' yamekosa tafsiri yake katika Kiswahili. Kulingana na Micaela (2008) katika tafsiri kuna changamoto ya maneno maalum ambayo yamejikita katika utamaduni wa LC na ambayo hayaeleweki katika LL ama hayapo kabisa katika LL. Micaele anaendelea kueleza kuwa matini ya kitamaduni inatafsiriwa kwa kutumia misamiati isiyosadifiana na maana na ujumbe wa matini chanzi na hivyo basi kupoteza maana iliyokusidiwa. Katika uchanganuzi huu, swala la kikwazo cha tafsiri kutokana na maneno ya utamaduni wa Kiingereza

ambayo hayana tafsiri mwafaka kwa Kiswahili limeweza kujitokeza. Kwa mujibu wa nadharia ya Isimu Kongoo, lugha hutoa maana yake kama tunavyoitumia kama wanajamii. Katika mifano iliyotolewa, maneno ya Kiingereza yanakosa tafsiri katika Kiswahili kwa sababu maneno haya yana asilia katika utamaduni wa Kiingereza.

### 3.1.4 Matatizo Katika Kiwango Cha Uhawilishaji

Zoezi la uhawilishaji huhakikisha kuwa kuna ulinganifu wa maana ya visawe katika LC na LL. Iwapo neno la kutafsiririwa linaweza kuwa na maana zaidi ya moja, basi mtafsiri ana jukumu la ziada la kuhakikisha kuwa uteuzi wa visawe vyake unakaribiana zaidi na maneno ambayo anayatafsiri. Visawe hivi lazima viwe na ujumbe na maana sawa na LC ili kufanikisha shughuli ya tafsiri. Katika utafiti wetu, tulijadili chanzo hiki cha tafsiri potovu na tukapima ulinganifu wa maana ya maneno katika LC na ile maana ambayo imejitokeza kama tafsiri katika LL na kutoa mapendekezo ya tafsiri bora. Jedwali 3.4 linaonyesha matatizo katika kiwango cha uhawilishaji.

**Jedwali 3.4: Matatizo Katika Kiwango Cha Uhawilishaji**

| **Neno la Kiingereza** | **Tafsiri katika Kamusi-tafsiri ya mtandaoni** | **Tafsiri bora** |
|---|---|---|
| Fool | Kumdanganya | mpumbavu |
| Job | Testi | Kazi |
| Joke | Furaha | Utani/Mzaha |

Neno 'Fool' katika Jedwali 3.4 limetafsiriwa kama kumdanganya badala ya mpumbavu, ijapokuwa kuna ukweli fulani katika tafsiri hii, tafsiri hii inaweza tu kukubalika katika muktadha ambao neno hilo 'fool' limetumika kumaanisha kuwa mtu amepigwa shere wala si mtu kama nomino. Neno 'Joke' limetafsiriwa kama

furaha. Katika maana ya kimsingi, neno joke linaweza tafsiriwa kama utani ama mzaha. Aidha, lazima ibainike wazi iwapo neno la kutafsiriwa ni la aina gani kwani aina ya maneno yanaathiri sana tafsiri. Shughuli ya uhawilishaji wa mawazo unahitaji kuhakikisha kuwa kuna ulinganifu wa maana na ujumbe wa visawe vya LC na LL, ili kuhakikisha kuwa ujumbe utakaotolewa kwenye LL ni sawia na ule kwenye LC (Jilala, 2014). Aidha, kulingana na mhimili wa nadharia ya Ulinganifu wa Kimuundo, maana jinsi ilivyokusudiwa katika lugha chanzi sharti ilingane na maana katika lugha lengwa.

### 3.1.5 Udurusu wa Kongoo- Matini Kutofanyika au Kufanyika Kiholela

Shughuli ya udurusu inarejelea hali ya kupitia makala fulani kwa nia ya kuhakikisha kuwa nakala hiyo haina makosa yoyote katika vitengo mbalimbali vya lugha. Jedwali 3.5 linaonyesha udurusu wa kongoo -matini kupuuzwa au kufanyika koholela.

**Jedwali 3.5: Udurusu wa kongoo – matini kupuuzwa au kufanyika koholela**

| **Neno la Kiingereza** | **Tafsiri katika Kamusi ya mtandaoni** | **Tafsiri bora** |
|---|---|---|
| Kettle | Aaa | Birika |
| Admiral | Muddyb | Yenye kupendeka |
| Mingling | Minglingly | Tangamana |

Katika Jedwali 3.5, neno ‘Kettle’ limetafsiriwa kama aaa badala ya birika. Neno ‘Admiral’ limetafsiriwa kama muddyb badala ya yenye kupendeka ilhali neno ‘Mingling’ limetafsiriwa kama minglingly badala ya tangamana. Katika mifano hii,

tafsiri iliyotolewa haina maana inayohusiana na maneno yanayotafsiriwa. Kulingana na majibu ya hojaji ya mtaalamu wa teknolojia, hili linaashiria wazi kuwa huenda udurusu wa kongoo-matini hukufanyika ama ulifanyika kiholela pakatokea aina hii ya upotovu katika tafsiri. Hili pia linaafiki tafsiri sahihi zilizo na mwendelezo mbaya wa maneno. Zoezi la tafsiri halikamiliki pasi na mtafsiri kubaini uhusiano kati ya MC na ML, ili kuhakikisha kuwa matini haya yana uhusianio wa karibu zaidi. Zoezi hili lina umuhimu sana katika tafsiri kwani ndilo linapima mfanano wa dhana na ujumbe kwenye MC na ML na kupima uhusiano wa makala haya mawili (Mwangi, 2016). Katika hatua hii, mtafsiri huwa na nafasi ya kusahihisha matini ambayo tayari ametafsiri huku akiwa na nia ya kukosoa makosa ya kimsamiati, kimuundo na ufasaha wa visawe alivyovitumia (Jilala, 2014). Udurusu huu ukifanyika kwa ufasaha na bila haraka kabla ya machapisho, unaweza kuepusha makosa ya tafsiri yanayoweza kujitokeza kwenye makala yaliyopigwa chapa.

### 3.1.6 Kutokuwepo Kwa Sera Za Kuhakikisha Uboreshaji Wa Kamusi- Tafsiri Za Mtandaoni Mara Kwa Mara

Kupitia kwa hojaji na majadiliano, utafiti huu ulibaini kwamba hakuna sera zozote za kuongoza wataalamu kuboresha kamusi-tafsiri ambazo tayari zipo kwenye mtandao. Baada ya kamusi hizi kupachikwa kwenye mtandao, shughuli hii huwa imeishia hapo wala hakuna mikakati yoyote ya kuzipekua tena baada ya muda fulani kuhakikisha kuwa ubora wao unadumishwa. Mawazo haya yaliungwa mkono na watafitiwa ambao walihusika moja kwa moja kupitia kujaza hojaji na vile vile kushiriki katika mahojiano jinsi inavyodhihirika katika Jedwali 3.6.

**Jedwali 3.6: Kutokuwepo Kwa Sera Za Kuhakikisha Uboreshaji Wa Kamusi-Tafsiri Za Mtandaoni**

| Hakuna sera za kuhakiki uboreshaji wa kamusi- tafsiri za mtandaoni | Waliokubaliana | Wasiokubaliana |
|---|---|---|
| Mwitikio wa waadhiri | 5 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |
| Mwitikio wa waalimu | 7 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |
| Mwitikio wa wanafunzi | 5 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |
| Mwitikio wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |

Jedwali 3.6 linaonyesha maoni ya watafiti waliokubaliana kuwa hakuna sera za kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni kulingana na majibu ya hojaji. Kwa mujibu wa Iribe Mwangi (1996), tafsiri yoyote ile huwa na makosa na hivyo basi, sharti kuwepo kanuni za kuhakiki ili kuhakikisha kuwa makosa yanayotokana na tafsiri hiyo yamerekebishwa.

### 3.1.7 Kutokuwa kwa Sera ya kuhakiki na kusawazisha Kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao

Jambo jingine lililotokea wazi katika utafiti huu ni swala la kutokuwa na sera ya kuongoza uhakiki wenye nia ya kusawazisha kongoo ya Kiingereza na ile ya Kiswahili katika kamusi- tafsiri za mtandaoni. Jedwali 3.7 linawasilisha data kuhusu swala hili baada ya uchunzaji.

**Jedwali 3.7: Kutokuwa Kwa Sera Ya Kuhakiki Na Kusawazisha Kongoo Ya Kiswahili Na Ya Kiingereza Kwenye Mtandao**

| **Hakuna sera za kuhakiki na kusawazisha Kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao** | **Waliokubaliana** | **Wasiokubaliana** |
|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |
| Mwitikio wa walimu | 7 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |
| Mwitikio wa wanafunzi | 5 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |
| Mwitikio wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 0 |
| Asilimia | 100 | 0 |

Kwa mujibu wa matokeo katika Jedwali 3.7, asilimia 100 ya watafitiwa walisema kuwa hakuna sera za kuhakiki. Uhakiki wa mara kwa mara utawezesha kudumisha ubora wa tafsiri na pia kufanya marekebisho yoyote ambayo yanastahili kufanywa ili kuboresha tafsiri. Madai haya yalitokana na kusawazisha Kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao. Kwa mujibu Jilala (2014), kazi ya kutafsiri si tukio tu bali ni shughuli inayoendelea. Kutokana na mtazamo huu, basi kuna haja ya kubuniwa kwa sera za kuhakiki na kusawazisha kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao kwa minajili ya kuboresha tafsiri ya kamusi-tafsiri za mtandaoni.

### 3.1.8 Upana Wa Maneno Na Kuzuka Kwa Misamiati Ya Kiingereza Na Kiswahili

Kiswahili, sawia na Kiingereza ni lugha inayokua kila uchao huku maneno mapya na misamiati ikiibuka kadri ya maendeleo ya mawanda mbalimbali ya kijamii. Kutokana na hali hii, tafsiri ya neno fulani huenda ikahitilafiana na tafsiri iliyotolewa awali na isiyoambatana na maendeleo haya katika jamii. Kwa mfano, tafsiri ya baadhi ya maneno hayazui maana halisi kama maneno hayo yanavyotumika kwa sasa bali yanazingatia tu maana ya kijumla ya hapo awali au hata tafsiri ya maneno haya kutokuwepo kabisa katika kamusi hizi. Jedwali 3.8 linaonyesha maneno ya Kiingereza ambayo hayana tafsiri katika Kiswahili.

**Jedwali 3.8: Maneno Ya Kiingereza Yasiyo Na Tafsiri Sambamba Ya Kiswahili**

| **Neno la Kiingereza** | **Tafsiri katika Kamusi ya mtandaoni** |
|---|---|
| Drinking basket/ Bucket | Ndoo |
| Ice skating | Ice skating |
| High Tea | High Tea |

Katika Jedwali 3.8, tafsiri ya maneno ‘Drinking basket/bucket’ imetolewa kijumla kama ndoo. Neno na ‘High tea’ limesalia vile vile kwani hakuna tafsiri ya neno hilo kwa Kiswahili. Kulingana na Mutugi (2012), tafsiri ni mchakato wala si tukio, hivyo basi mchakato huo sharti uzingatiwe kikamilifu ili kupata tafsiri inayofaa. Kwa mfano, mchakato huo sharti uzingatie kuzuka kwa msamiati mpya katika lugha husika, Kiingereza au Kiswahili katika muktadha huu. Kulingana na mhimili wa

nadharia ya Isimu Kongoo, lugha hutoa maana yake kama tunavyoitumia kama wanajamii na hivyo basi, tafsiri sharti itilie maanani utamaduni wa LC na LL ili kuleta maana inayowiana.

### 3.1.9 Swala La Lugha Ya Kiswahili Kukua

Kiswahili ni lugha inayokua kila uchao na hali hii inawahitaji waandalizi wa kamusi tafsiri za mtandaoni kuwa mstari wa mbele katika kufahamu maneno na misamiati mipya inayoibuka kila uchao. Ukuaji wa lugha ya Kiswahili unamaanisha kuwa misamiati inaibuka na kuibuliwa kila uchao ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya matumizi ya lugha. Utafiti huu ulibaini kuwa kuna baadhi ya maneno yanayoibuka na kupata tafsiri bora zaidi jinsi inavyojitokeza katika Jedwali 3.9.

**Jedwali 3.9: Swala La Lugha Ya Kiswahili Kukua**

| Neno la Kiingereza | Tafsiri katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni | Tafsiri bora |
|---|---|---|
| Atheist | Asiyeamini Mungu | Mkanamungu |
| Scanner | Skana | Mdaki |

Japo neno asiyeamini Mungu linahusiana na neno ‘Atheist’, neno hilo limewekwa katika muktadha wa sentensi ambapo linaonekana kufafanua maana ya neno jingine. Neno ‘Scanner’ limetoholewa moja kwa moja na kutafsiriwa katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni kama skana. Utohozi wa maneno hufanyika pale ambapo neno mwafaka hukosa katika LL. Katika mfano huu, neno la Kiswahili linalolingana na ‘Scanner’ ni mdaki. Ukuaji wa lugha ya Kiswahili unamaanisha kuwa misamiati inaibuka na kuibuliwa kila uchao ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya matumizi ya

lugha. Swala hili linaweza kuwa changamoto na kuzua hali ya kupakia kwa tafsiri potovu ya maneno haya kwenye kamusi za mtandaoni.

### 3.1.9 Makosa ya kiufundi; kikagua tahajia

Kulingana na hojaji ya mtaalamu wa teknolojia, jambo jingine ambalo lilijitokeza katika utafiti huu ni kuwa kuna tafsiri isiyo bora zaidi kutokana na kikagua-tahajia kusoma visivyo baadhi ya maneno na hivyo kuyatafsiri visivyo. Madai haya yalitolewa na mtafitiwa mmoja ambaye ni mtaalamu anayehusika katika maandalizi ya programu za kamusi za mtandaoni. Kulingana na maoni ya mtafitiwa huyo, iwapo kikagua tahajia hakitaweza kusoma vyema maneno ya Kiingereza au visawe vya maneno haya, basi kinaweza kikakosa kutoa tafsiri sahihi ya hayo maneno. Jedwali 3.10 linaonyesha baadhi ya maneno ambayo huenda yametafsiriwa visivyo kutokana na makosa ya kiufundi.

**Jedwali 3.10: Tafsiri potovu kutokana na makosa ya kiufundi**

| Neno la Kiingereza | Tafsiri katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni | Tafsiri bora |
|---|---|---|
| Mouth | Musings | Mdomo |
| Millionaire | Millionary | Milionea |
| Mingling | Minglingly | Tangamana |

Katika Jedwali 3.10, neno ‘Mouth’ limetafsiriwa katika Kiswahili kama ‘musings’, neno ‘Millionaire’ kama ‘Millionary’ na neno ‘Mingling’ kama ‘Minglingly’. Maneno yaliyotafsiriwa katika Kiswahili si ya Kiswahili wala hayana maana inayohusiana na yale ya Kiingereza. Kongoo Sambamba ni kongoo inayotumika

katika mazingira ya matini ya uwili lugha na ambayo inajikita katika kulainisha visawe vya tafsiri za lugha husika. Kulingana na Ipara (2008), lugha ya Kiswahili ni lugha ya kimataifa ambayo inafaa kusambazwa kwa ufasaha ili kuwafaidi wale wanaotegemea kujifunza au kuitumia kwa njia moja au nyingine. Hivyo basi, makosa ya kiufundi katika tafsiri yanafaa yawe ya kiwango cha chini. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Isimu Kongoo, muundo na maana haviwezi tenganishwa.

### 3.1.10 Makosa Kutokana na Hali/ Mambo Mengineyo

Baadhi ya makosa huweza kusababishwa na machovu ya wataalamu wanapochapisha maneno katika harakati ya kujenga kongoo ya kamusi hizi. Pia, kazi ya tafsiri mtandaoni na ujenzi wa kamusi za mtandaoni huweza kufanywa na mtu yeyote, bila kujali utaalamu wao ama kiwango chao cha utalaamu wa lugha ya Kiswahili. Jambo hili limesababisha kupakia maneno ambayo huenda yakafanana na tafsiri sahihi lakini sio tafsiri mwafaka. Kwa mujibu wa Jilala (2014), tafsiri yoyote ile sharti ihusishe wataalam wa lugha na vile vile wahariri. Naye Larson (1984) anadokeza kuwa sharti tafsiri ifanyiwe usawidi ili kurekebisha makosa na kujumuisha maoni yaliyopendekezwa na wahariri.

## 3.2 Viwango Anuai vya Makosa Vilivyoathiri Ubora Wa Tafsiri

Sehemu hii inaangazia viwango anuwai vya makosa vilivyoathiri ubora wa tafsiri. Kwa mujibu wa ufatifi huu, viwango hivyo ni pamoja na: makosa katika viwango vya mofolojia, semantiki na pragmatiki.

### 3.2.1 Makosa Katika Kiwango cha Mofolojia

Mofolojia ni taaluma ya isimu ambayo huchunguza maumbo ya maneno kwa mujibu wa Mathews, (1974). Wanaisimu wengi wamekubali kuwa mofolojia inaweza

kugawanywa katika matawi mawili makuu ya Mofolojia ya minyambuliko ya maneno na Mofolojia ya Uundaji wa maneno. Mofolojia ya minyambuliko ya maneno hushughulikia minyambuliko ya maneno kwa kuzingatia viambishi vinavyoongezwa kwenye mizizi ya maneno ili kuwakilisha maana mbalimbali lakini minyambuliko hiyo isibadili aina ya neno hilo (Mgullu, 1999). Mofolojia ya uundaji wa maneno kwa upande mwingine ni eneo linaloshughulikia mikondo ya matokeo ya kiisimu ya uundaji wa maneno kwa kuweka viambishi katika mizizi ya maneno.

Jambo La msisitizo hapa ni kuwa wakati viambishi mbalimbali vinapoongezwa katika mzizi wa neno, tunapata neno jipya. Jedwali 3.11 linaonyesha makosa katika kiwango cha mofolojia.

**Jedwali 3.11: Makosa Katika Kiwango Cha Mofolojia**

| **Neno la Kiingereza** | **Tafsiri katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni** | **Tafsiri bora** |
|---|---|---|
| Delete | Ku-futa | Futa |
| Class | Darasa-ni | Darasa |

Katika Jedwali 3.11, neno ‘Class’ limetafsiriwa kama darasani ambapo nomino darasa imeongezewa kihusishi -ni na kulipa neno hilo maana ya ndani ya darasa badala ya darasa. Vile vile, neno ‘Delete’ limeongezewa kiambishi ku- na kulipa maana tofauti na ile ya kimsingi iliyokusudiwa. Kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu, tafsiri bora ni ile ambayo maumbo ya maneno mapya yanayotumiwa kama tafsiri yanapaswa kuoana kimaana na maneno ya Kiingereza na hivyo, maumbo yasiyofaa yakitumika basi yanaathiri ubora wa tafsiri. Kwa kurejelea mhimili wa

nadharia ya Ulinganifuwa Kimuundo, kongoo ya LC inapaswa kuwiana na muundo wa LL ili kutimiza malengo ya tafsiri.

### 3.2.2 Makosa Katika Kiwango Cha Semantiki

Kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990), Semantiki inaelezwa kuwa tawi la isimu ambalo hushughulikia maana katika lugha. Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha (2004) inaeleza semantiki kuwa kama taaluma inayojishughulisha na uchunguzi na uchambuzi wa maana za maneno au tungo katika lugha. Katika utafiti huu, baadhi ya tafsiri zilionekana kukiuka sheria za kisemantiki na hivyo kuwa potovu kwa kuzingatia semantiki-leksia inayochunguza maana kwa kiwango cha neno, kwa kuzingatia mzizi wa neno hilo. Jedwali 3.12 linaonyesha data iliyochanganuliwa kuhusu swala hili.

**Jedwali 3.12: Makosa katika kiwango cha Semantiki**

| Neno la Kiingereza | Tafsiri katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni | Tafsiri bora |
|---|---|---|
| Bitter | Uchungu | Chungu |
| Brick | Matofali | Tofali |

(The English- Swahili Dictionary)

Katika Jedwali 3.12, neno ‘Bitter’ limetafsiriwa kama uchungu katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni. Licha ya kuwa kuna uhusiano wa kimaana katika tafsiri hii, kwa kuzingatia mzizi wa neno la Kiingereza, tafsiri ya neno hili katika Kiswahili ni chungu wala si uchungu. Neno la Kiingereza linalowiana kimaana na uchungu ni ‘bitterness’. Ili tuseme kuwa tafsiri iliyotolewa ni sahihi, basi leksia ya neno-tafsiri inapaswa kuwa na maana sawa na la Kiingereza. Kwa kurejelea nadharia ya Isimu Kongoo, muundo na maana havifai kutenganishwa jambo ambalo linaonekana

kukiukwa katika mifano ya tafsiri inayorejelewa katika sehemu hii. Hili linapewa uzito na dhana ya kwamba maneno au mwambatano wa maneno unadokeza maana fulani (Chacha, 2019).

### 3.2.3 Makosa katika Kiwango cha Pragmatiki

Pragmatiki ni tawi la kiisimu linalichunguza maana ya neno katika muktadha ambamo neno hilo limetumika. Katika kukagua ubora wa neno-tafsiri, maana ya tafsiri hiyo kama inavyojitokeza katika sentensi kwa kuzingatia neno lake la Kiingereza haiwezi kupuuzwa. Neno lake la Kiingereza lazima lioane na maana ya tafsiri yake katika muktadha wa sentensi ili tuseme kuwa tafsiri hiyo ni bora, la sivyo kosa la kutozingatia kitengo cha kipragmatiki hutokea. Jedwali 3.13 linaonyesha makosa katika kiwango cha pragmatiki.

Jedwali 3.13 linaonyesha mfano wa makosa katika kiwango cha pragmatiki. Pragmatiki inahusika na maingiliano ya ufahamu wa kisemantiki na ufahamu wetu kuhusu ulimwengu huku muktadha wa matumizi ukizingatiwa (Malangwa, 2019). Mofolojia inahusiana na maumbo ya maneno na hivyo, iwapo neno-tafsiri ambayo ni kongoo kwenye mtandao ikiwa na maumbo mabovu basi kosa hili linachambuliwa kwa misingi ya kimofolojia. Hili linaweza kutokana na kikagua-tahajia kukosa kulikosoa neno hili. Katika misingi ya kisemantiki, neno la Kiingereza huenda likawa na tafsiri yake sahihi ya Kiswahili lakini likapewa neno tofauti kabisa kimaana kama tafsiri yake. Mwisho, iwapo neno la Kiingereza linaweza kuwa na tafsiri zaidi ya moja, basi lazima tafsiri ya Kiswahili izingatie muktadha ambamo LL inanuia kutumia tafisi hiyo. Tazama jedwali linavyotoa ufupi wa maelezo haya.

**Jedwali 3.13: Makosa Katika Kiwango Cha Pragmatiki**

| Taaluma | Mofolojia | Semantiki | Pragmatiki |
|---|---|---|---|
| **Ukiukaji wake** | - Tafsiri/neno sahihi<br>- Maumbo potovu | - Maana potovu<br>- Maumbo sahihi | - Neno sahihi<br>- Maana potovu kimuktadha |

Hivyo basi, utafiti huu ulibaini kuwa matumizi ya baadhi ya tafsiri yanakiuka ufahamu wetu wa neno-tafsiri katika muktadha wa matumizi ya maneno hayo.

### 3.3 Hitimisho

Sura hii imesheheni kiwango cha muhimu sana katika utafiti wetu kwani imeweza kujibu lengo la utafiti la kubaini vyanzo vya tafsiri potovu kwenye kamusi-tafsiri za mtandaoni. Utaifi uliweza kupata kuwa tafsiri potovu imetokana na mambo mengi yakiwemo: Tofauti za Muundo wa lugha ya Kiswahili na muundo wa Lugha ya Kiingereza, tofauti za kimitindo kati ya Lugha ya Kiswahili na Kiingereza, matatizo ya uteuzi wa msamiati au maneno maalum, matatizo katika kiwango cha uhawilishaji, na udurusu wa Kongoo- Matini kupuuzwa au kufanyika kiholela. Mbali na hayo, vyanzo vingine vilivyoibuka ni kutokuwepo kwa sera za kuhakikisha uboreshaji wa Kamusi- tafsiri za mtandaoni mara kwa mara, kutokuwa kwa Sera ya kuhakiki na kusawazisha Kongoo ya Kiswahili na ya Kiingereza kwenye mtandao upana wa maneno kuzuka kwa misamiati ya Kiingereza na Kiswahili na makosa ya kiufundi yanayotokana na kikagua tahajia.

Mbali na hayo, tumeweza kuchanganua upotovu wa tafsiri kwa kuzingatia vigezo vya kiisimu vya Mofolojia, Sintaksia na Pragmatiki na kuonyesha jinsi kanuni zao zilivyokiukwa katika kutoa maneno-tafsiri kwenye kamusi–tafsiri za mtandaoni. Katika sura inayofuata, utafiti wetu umejaribu kutoa mapendekezo ya mikakati au namna ya kuboresha kamusi hizi kwa kutumia mbinu za hojaji na mahojiano.

# SURA YA NNE

# MIKAKATI YA KUBORESHA KAMUSI-TAFSIRI ZA MTANDAONI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu, utafiti huu umeangazia vyanzo vya tafsiri potovu kwenye kamusi-tafsiri za mtandaoni. Ilibainika kuwa kuna vyanzo vingi vinavyosababisha tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Sura hii ya nne iliangazia mikakati ya kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni kwa kuzingatia mihimili ya nadharia zinazoongoza utafiti huu ambazo ni Isimu Kongoo na ile ya Ulinganifu wa Kimuundo. Mikakati hiyo ni kama vile kubuniwa kwa sera ya kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni, udurusu wa kongoo-matini kufanywa kwa ufasaha, kujumuisha wataalamu wa lugha katika maandalizi ya kongoo-matini, ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara, ujumuishaji wa idara ya lugha vyuoni katika kuandaa kongoo matini, udurusu wa kamusi–tafsiri mitandaoni kufanywa mara kwa mara, kutathmini utendakazi wa kikagua tahajia mara kwa mara, na kuongeza nguvu-kazi ya wahariri.

## 4.1 Mikakati Iliyojitokeza ya Kuboresha Kamusi-Tafsiri za Mtandaoni

Mikakati iliyoangaziwa katika utafiti huu ni ile kama iliyopendekezwa katika data za mahojiano, hojaji na usomaji wa maktabani. Kwa kuwa kamusi za mtandaoni zimekuwa zenye manufaa makuu kwa jamii na haswa kwa wapenzi wa Kiswahili, uboreshaji wazo utafidia mapungufu yanayotokana na matumizi ya kamusi halisia. Mojawapo ya mapungufu hayo ni kuwa ingemlazimu mtumiaji kukibeba kitabu chenyewe kokote ili aweze kukitumia lakini kwa sasa anaweza akachakura tu neno alitakalo kupitia simu ya mkononi popote alipo. Pia uboreshaji wa kamusi hizi utafanikisha shughuli ya kutafsiri vitabu vya mtandaoni almaarufu *e-books*

vinavyotegemea kamusi hizi ili kutafsiri makala yao. Iwapo mtumiaji wa kamusi-tafsiri hizi si mwanaafrika mashariki aliye na uwezo wa kubaini tafsiri bora au potovu, basi lengo kuu la makala yake anayoyatafsiri huenda likapotea. Mbali na hayo, wanaotafuta tafsiri ya maneno kwa matumizi yao ya kibinafsi wana haki ya kupata makala bora ili wasipotoke. Sehemu hii imechanganua mikakati mbalimbali ya kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni. Kupitia uchunzaji wa mahojiano na hojaji, utafiti ulibaini kuwa kuna mikakati kadhaa inayofaa kuzingatiwa ilikuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni.

### 4.1.1 Kubuniwa Kwa Sera ya Kuhakiki Kamusi-tafsiri za Mtandaoni

Kamusi tafsiri zinapokamilika kuratibiwa, hatua ya mwisho huwa kuzipakia kwenye mtandao ili watumizi wake wakazitumie moja kwa moja. Sehemu ifuatayo imewasilisha data ya mahojianoya moja kwa moja na uchunzaji uliofanyika ukiwashirikisha wahadhiri wa Chuo Kikuu, waalimu wa shule ya upili, wanafunzi wa uzamili na mtaalam wa teknolojia walitoa maoni yao muhusu kubuniwa kwa sera ya kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni kama inavyodhihirika katika Jedwali 4.1

**Table 4.1: Kubuniwa Kwa Sera Ya Kuhakiki Kamusi-Tafsiri Za Mtandaoni**

| **Sera za kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni zibuniwe** | **Waliotilia maanani** | **Asilimia (%)** | **Wasiokubaliana** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 4 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa walimu wa shule za upili | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Jedwali 4.1 linaonyesha kuwa wahojiwa wote asilimia 100 walikubaliana kuwa kuna haja ya kubuniwa kwa sera ya kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni. Kubuniwa kwa sera hizi kunafaa ili kuhakikisha kuwa makala yanayopakuliwa kama kongoo – tafsiri ni sahihi. Hili lilitoka na hali ya kuwa baada ya kongoo hupakuliwa mtandaoni kama kamusi–tafsiri, hapana juhudi nyingine ya kuhakikisha kuwa kongoo iliyopakiwa ni sawa na ile inayopakuliwa. Jilala (2014) anaeleza kuwa kazi ya tafsiri si tukio tu bali ni shughuli ambayo hufuata hatua kadhaa zinazotilia maanani sera za tafsiri. Sera hizi zinafaa kuhusisha wataalamu wa mtandao wa *google* ambao watakuwa wakihakiki programu hizi kila baada ya muda fulani na hivyo kuhakikisha kuwa kamusi hizi zinasalia katika hali bora ya matumizi. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Ulingalifu wa Kimuundo, uhakiki wa vifaa hivi utachangia katika

kuhakikisha kuwa maana jinsi inavyokusudiwa katika lugha chanzi inalingana na maana katika lugha lengwa.

### 4.1.2 Udurusu wa Kongoo- Matini Kufanywa kwa Ufasaha

Sehemu inayofuata inawasilisha data kuhusu watafitiwa walioshiriki katika kutoa mapendekezo kuhusu mikakati inayofaa kuchukuliwa ili kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni inavyojitokeza katika Jedwali 4.2.

| **Udurusu wa kongoo-matini kufanywa kwa ufasaha** | **Waliotilia maanani** | **Asilimia (%)** | **Wasiokubaliana** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa walimu wa shule za upili | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

**Jedwali 4.2: Udurusu Wa Kongoo- Matini Kufanywa Kwa Ufasaha**

Kwa mujibu wawatafitiwa, udurusu wa kongoo- matini unafaa kufanywa kwa ufasaha. Udurusu huu ukifanywa kwa ufasaha basi baadhi ya makosa kama vile yale ya mwendelezo wa maneno-tafsiri huweza kutatuliwa na hivyo kuboresha tafsiri. Mabeya (2012) anaeleza kuwa kuna haja ya kubadilisha mbinu za uundaji wa misamiati inayohifadhiwa kama kongoo-matini katika kamusi-tafsiri za mtandaoni ambapo anatoa mfano wa mbinu iliyotimika kuifadhi kongoo-matini inayotumika kama tafsiri kwa maneno inavyoathiri ubora wa tafsiri katika mradi wa *Microsoft*

*East Africa*. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Isimu Kongoo, muundo na maana haviwezi tenganishwa.

### 4.1.3 Kujumuisha Wataalamu Wa Lugha Katika Maandalizi Ya Kongoo-Matini

Kuandaa kamusi pamoja na vitabu vingine vya mtandaoni ni kazi ya kiufundi inayohusisha wajuzi wengi wakiwemo wale wa teknolojia. Kulingana na mahojiano yaliyofanyika na baada ya uchunzaji, Jedwali 4.3 linaonyesha data ya wahojiwa kuhusu kujumuisha kwa wataalamu wa lugha katika maandalizi ya kongoo- matini.

**Jedwali 4.3: Kujumuisha Wataalamu Wa Lugha Katika Maandalizi Ya Kongoo- Matini**

| Kujumuisha wataalamu wa lugha katika maandalizi ya kongoo-matini | Waliotilia maanani | Asilimia (%) | Wasiokubaliana | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa walimu wa shule za upili | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.3, wahojiwa wote asilimia 100 walikubaliana kuwa wataalamu wa lugha wajumuishwe katika maandalizi ya kongoo- matini ili kuepuka kiwango kikubwa cha upotovu katika tafsiri. Kulingana na maoni ya mtaalamu wa teknolojia, hakuna nafasi iliyotengewa wataalamu wa lugha ili wakague kamusi-tafsiri za mtandaoni kabla hazijapachikwa mtandaoni. Kwa mujibu wa Jilala (2014), kushirikishwa kwa wataalamu lugha katika tafsiri ni moja kati ya hatua ambazo sharti zichukuliwe ili kupata tafsiri bora. Hili linamaanisha kuwa tafsiri bora inahitaji mchango wa wataalamu lugha ili kuifanikisha.

### 4.1.4 Ujumuishaji Wa Maneno Mapya Mara Kwa Mara

Watafitiwa walitakiwa kutoa maoni kuhusu ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara katika kuimarisha tafsiri ya kamusi-tafsiri za mtandaoni. Baada ya mahojiano na watafitiwa hao uchunzaji kufanyika na  data imewasilishwa katika Jedwali 4.4.

**Jedwali 4.4: Ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara**

| **Ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara** | **Waliotilia maanani** | **Asilimia (%)** | **Wasiokubaliana** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa walimu wa shule za upili | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Jedwali 4.4 linaonyesha kuwa wahojiwa wote asilimia 100 wana mtazamo kuwa ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara katika kamusi-tafsiri ya mtandaoni unahitajika. Hii ni muhimu ili kuziba mwanya uliopo kwa sababu ya kutumia tafsiri ile ile ya maneno kongwe kwa maneno au misamiati mipya. Baadhi ya maneno au misamiati ambayo imetafsiriwa visivyo ni ya maneno ambayo yameibuka hivi karibuni na kongoo kuandaliwa kabla ya utafiti wa kutosha kufanyika kuhusu tafsiri yayo. Kulingana na mhimili wa nadharia ya Isimu Kongoo, lugha hutoa maana yake kama tunavyoitumia kama wanajamii na hivyo basi, kuna haja ya kuhakikisha kuwa misamiati mipya inatafsiriwa ipasavyo.

### 4.1.5 Ujumuishaji Wa Idara Ya Lugha Vyuoni Katika Kuandaa Kongoo Matini

Jedwali 4.5 linadokeza data iliyotokana na mahojiano na watafitiwa kuhusu ujumuishaji wa idara ya lugha vyuoni katika kuandaa kongoo matini.

**Jedwali 4.5: Ujumuishaji Wa Idara Za Lugha Ya Kiswhili Vyuoni Katika Kuandaa Kongoo Matini**

| Ujumuishaji wa idara ya lugha vyuoni katika kuandaa kongoo matini | Waliotilia maanani | Asilimia (%) | Wasiokubaliana | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa waalimu | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Katika Jedwali 4.5, asilimia kubwa yawatafitiwa walikua na mtazamo kuwa ujumuishaji wa idara ya lugha vyuoni katika kuandaa kongoo matini katika kamusi-tafsiri za mtandaoni unafaa. Hata hivyo, mtafitiwa mmoja alitoa maoni yaliyokinzana na wengine akisema kuwa kunafaa kubuniwa majopo maalum ya kitaifa kufanya shughuli hiyo. Maandalizi ya kongoo-matini ni shughuli ambayo si rahisi kutekeleza. Kulingana na maoni yaliyotolewa na wahojiwa, mchakato wote

unaohusika unachukua muda wa miezi mingi hadi mwaka kabla kongoo fulani kuwa tayari kutumika katika programu husika. Hata hivyo, katika harakati hii, wadau huenda wakabanwa na muda na kuishia kufanya kazi kiholela na kutowahusisha wadau ambao mchango wao huenda ukawa wenye manufaa zaidi. Kwa mujibu wa Jilala (2014), tafsiri ina hatua kadhaa ambazo sharti zifuatwe ili iwe bora. Ujumuishaji wa idara za lugha ni muhimu kwa sababu wahadhiri na walimu katika idara hizo ni wataalam wanaojihusisha na maswala ya lugha. Idara za Lugha ya Kiswahili vyuoni zinaweza kubuni vitengo vya kushughulikia kongoo-matini iwapo wataweza kuhusishwa na kampuni zinazoandaa kamusi – tafsiri za mtandaoni. Kazi kuu ya idara hizi kwenye vyuo anuai itakuwa kukagua kongoo na kuhakikisha kuwa tafsiri mwafaka imetolewa kwani wao ni wataalamu wa lugha wala si wataalamu wa teknolojia kama walivyo waandalizi wa programu zenyewe.

### 4.1.6 Udurusu Wa Kamusi –Tafsiri Mitandaoni Kufanywa Mara Kwa Mara

Wahojiwa walihitajika kutoa maoni yao kuhusu udurusu wa kamusi-tafsiri za mitandaoni kufanywa mara kwa mara. Jedwali 4.6 linaonyesha matokeo ya maoni ya wahojiwa hao.

**Jedwali 4.6: Udurusu Wa Kamusi-Tafsiri Ya Mitandaoni Kufanywa Mara Kwa Mara**

| **Udurusu wa kamusi-tafsiri ya mitandaoni kufanywa mara kwa mara** | **Waliotilia maanani** | **Asilimia (%)** | **Wasiokubaliana** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa waalimu | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Jedwali 4.6 linaonyesha kuwa asilimia 100 ya walitoa maoni kuwa udurusu wa kamusi-tafsiri za mtandaoni unafaa kufanywa mara kwa mara. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ilibainika kuwa baada ya kamusi-tafsiri hizi kuwa tayari na kupakiwa mtandaoni, hakuna juhudi zozote zinazofanywa ili kuziboresha. Jilala (2014) anaeleza kuwa udurusu wa rasimu ya kwanza na ya mwisho ya tafsiri ni mojawapo ya hatua muhimu katika shughuli ya tafsiri. Juhudi za tafsiri zinahusiana na udurusi wa kongoo-matini na kuhakikisha kuwa tafsiri hiyo imesalia kuwa bora almuradi kamusi hizi zinazidi kutumika.

### 4.1.7 Kutathmini Utendakazi Wa Kikagua Tahajia Mara Kwa Mara

Kikagua-tahajia kina umuhimu mkubwa katika mandalizi ya vitabu au makala ya mtandaoni kwani kinahakikisha kuwa mwendelezo wa maneno unafaa na hivyo

makala kuwafaa zaidi watumizi wake. Jedwali 4.7 linaonyesha data baada ya uchunzaji kutokana na mahojiano yaliyofanyika na watafitiwa.

**Jedwali 4.7: Kutathmini Utendakazi Wa Kikagua Tahajia Mara Kwa Mara**

| Kutathmini utendakazi wa kikagua tahajia mara kwa mara | Waliotilia maanani | Asilimia (%) | Wasiokubaliana | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa waalimu | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.7, watafitiwa wote asilimia 100 walikuwa na mtazamo kuwa kutathmini utendakazi wa kikagua tahajia mara kwa mara kunafaa. Kulingana na mtaalam wa teknolojia, utathmini wa utendakazi wa kikagua tahajia huwa haufanyiki mara kwa mara. Hivyo basi, kifaa hiki kikiwa na dosari, makosa ya hapa na pale hayawezi kuepukika. Vilevile, kutokana na majibu ya hojaji ya utafiti, kulikuwa na pendekezo kuwa ni vyema pawe na mikakati ya kutathmini utendakazi wa kifaa hiki mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa kinafanya kazi vilivyo na kwamba hakitoi mwanya wowote na kusababisha makosa katika kongoo-matini na hivyo basi kuipa tafsiri dosari. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Isimu Kongoo, maana jinsi ilivyokusudiwa katika lugha chanzi sharti ilingane na maana

katika lugha lengwa. Kulingana na Kihore (2002), programu ya kuingisha lugha katika tarakilishi inafaa kuboreshwa kwa minajili ya kumwezesha mtumiaji kuchanganua data akitumia lugha ya Kiswahili badala ya Kiingereza. Iwapo kikagua tahajia kitafanya kazi ipasavyo basi tafsiri potovu inayotokana na mwendelezo mbaya wa maneno itaepukwa.

### 4.1.8 Kuongeza Nguvu-Kazi Ya Wahariri

Wahojiwa walihitajika kutoa maoni yao kuhusiana na kuongeza nguvu-kazi ya wahariri. Jedwali 4.8 linaonyesha matokeo kutokana na mahojiano hayo.

**Jedwali 4.8: Kuongeza Nguvu-Kazi Ya Wahariri**

| **Kuongeza nguvu-kazi ya wahariri** | **Waliotilia maanani** | **Asilimia (%)** | **Wasiokubaliana** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Mwitikio wa wahadhiri | 5 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitikio wa waalimu | 7 | 100 | 0 | 0 |
| Mwitiko wa wanafunzi | 5 | 100 | | 0 |
| Mwitiko wa mtaalamu wa teknolojia | 1 | 100 | 0 | 0 |

Jedwali 4.8 linaonyesha kuwa asilimia 100 ya wahojiwa walionelea kuwa ni muhimu kuongeza nguvu-kazi ya wahariri. Ni bayana kuwa kuna upungufu mkubwa ya nguvu –kazi na haswa ukiegemea maswala ya tafsiri kutokana na tafsiri potovu inayojitokeza katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Ili kamusi tafsiri hizi ziwe bora zaidi, kutahitajika wafanyikazi anuai kama vile wataalamu na watafiti wa Kiswahili

wanaokusanya na kusawazisha tafsiri, wanateknolojia wa kuzikarabati programu za kamusi mara kwa mara, na wahariri wanaosanifisha kongoo-tafsiri zinazopakiwa kwenye mtandao. Jilala (2014) anaeleza kuwa kuhariri kazi baada ya kutafsiri ili kuhakikisha kuwa matini chanzi inalingana na matini lengwa ni moja kati ya hatua zinazofaa kuzingatiwa katika kazi ya tafsiri. Shughuli ya uhariri ni ya umuhimu mkuu sana kwani ndiyo inayohakikisha kuwa tafsiri inayopakiwa ndiyo sahihi na wala haina makosa kama vile yale ya mwendelezo wa maneno. Kukiwa na uhaba wa wahariri, basi wale wachache hufanya kazi kiholela kwa nia ya kumaliza haraka wala si kwa nia ya kuwa na kazi bora.

## 4.2 Hitimisho

Sura hii imedokeza lengo la tatu na la mwisho la utafiti huu ambalo ni mikakati inayoweza kutumika ili kuboresha kamusi-tafsiri za mitandaoni. Sura hii imejadili baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni. Iwapo mapendekezo haya yatatiliwa maanani basi kamusi hizi zitazidi kuwa na manufaa zaidi kwa watumizi wake wa viwango na maeneo tofauti ulimwenguni. Mikakati ambayo imeangaziwa ni kama vile: Kubuniwa kwa sera ya kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni, udurusu wa Kongoo-Matini kufanywa kwa ufasaha, kujumuisha wataalamu wa lugha katika maandalizi ya Kongoo- Matini, ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara, ujumuishaji wa Idara za Lugha vyuoni Katika kuandaa Kongoo matini, udurusu wa Kamusi-Tafsiri mitandaoni Kufanywa mara kwa mara, kutathmini utendakazi wa kikagua tahajia mara kwa mara na kuongeza nguvu-kazi ya wahariri.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ya nne iliangazia mikakati ya kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni. Ilibainika kuwa kuna baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa minajili ya kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni. Sura hii inatamatisha utafiti wetu. Yaliyoangaziwa katika sura hii ni pamoja na muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti na mapendekezo ya tafiti zijazo.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini kamusi-tafsiri za mtandaoni kwa nia ya kudondoa tafsiri potovu kwa baadhi ya maneno ya Kiingereza na kujaribu kutafuta kiini cha upotovu huu kwenye kamusi-tafsiri hizi. Mbali na kutafiti kuhusu chanzo cha tafsiri potovu, lengo jingine lilikuwa kupendekeza mikakati ambayo ikizingatiwa inaweza kuboresha kamusi-tafsiri hizi. Aidha lengo lingine lilikuwa ni kupendekeza maneno ambayo huenda yakawa tafsiri bora zaidi kwa maneno yaliyotolewa kwa nia ya kuboresha kamusi ambazo zitaandaliwa siku za usoni.

Katika sura ya kwanza, msingi wa utafiti uliwekwa kwa kudurusi kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu kisha upeo na mipaka ya utafiti huu ukawekwa wazi na baadaye maswali ya utafiti yakaangaziwa. Mbali na haya, sababu za kuchagua mada hii ya ubora wa tafsiri unaodhihirika katika kamusi-tafsiri za mtandaoni zimetolewa. Utafiti huu aidha uliongozwa na nadharia mbili, ambazo ni nadharia ya tafsiri na nadharia ya Isimu–Kongoo na nadharia ya tafsiri ya Ulinganuifu wa Kimuundo. Nadharia hizi zimeelezwa kwa kina katika sura hii na tumeweza kuchanganua data yetu kwa misingi ya nadharia hizi. Lengo la kwanza la

utafiti huu limeshughulikiwa katika sura ya pili huku lengo la pili likishughulikiwa katika sura ya tatu. Lengo la tatu ambalo ndilo lengo la mwisho limeshughulikiwa katika sura ya nne kabla ya kutoa mahitimisho katika sura hii. Lengo la kwanza lilikuwa akubaini tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni na kupendekeza tafsiri mbadala, la pili likawa kubaini kiini cha tafsiri –potovu hii na la tatu likawa mikakati ya kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni.

Uti wa mgongo wa utafiti huu ulitokana na hali ya kuwepo zana za kuunda na kutathmini kamusi za kikompyuta. Hata hivyo, katika mipaka ya utafiti huu, kifaa hiki hakikaguliwi bali maneno ambayo tayari yamepachikwa katika kamusi-tafsiri za mtandaoni yalikaguliwa. Katika kujibu swali la tatu, utafiti huu umefafanua nafasi ya kongoo-matini kwani ndiyo nyenzo inayotumika kama malighafi ya maneno ya kamusi-tafsiri za mtandaoni. Iwapo kongoo-matini ni sahihi, basi kuna uwezekano mkubwa kuwa tafsiri nayo itakuwa sahihi. Katika hali hii, nadharia ya Isimu Kongoo iliyoasisiwa na John Sinclair (1982) na wenzake imefaa zaidi kwani nadharia hii inajihusisha moja kwa moja na maswala ya kongoo-matini ambapo tafsiri tunayoitathmini ni aina ya kongoo. Nadharia ya ulinganifu wa muundo nayo imetufaa kwa mapana kwani mihimili yake imetuwezesha kulinganisha na kulinganua kongoo ya lugha ya Kiingereza na ile ya Kiswahili ili kuwe na kigezo cha kutathmini usahihi au upotovu wa kongoo- tafsiri.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kubaini jinsi tafsiri isiyobora inavyoathiri mambo mbalimbali yanayohusiana na usomi au utafiti wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na kubainisha tafsiri potovu katika kamusi za mtandaoni, kujadili vyanzo vya tafsiri potovu kwenye kamusi za mtandaoni na kupendekeza mikakati ya kuboresha tafsiri

bora inayoweza kutumika katika kamusi-tafsiri za mitandaoni. Mbinu za mahojiano, hojaji na maktabani zilitumika katika kupata matokeo ya utafiti huu. Matokeo yafuatayo yalibainika katika kujadili malengo haya.

### 5.3.1 Kubainisha Tafsiri Potovu katika Kamusi-tafsiri za Mtandaoni

Utafiti huu ulibainisha kuwa kuna tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Misingi ya nadharia ya Isimu-Kongoo na nadharia ya tafsiri ya Ulinganuifu wa Kimuundo imetumika katika kuchangua data. Kwa kuangazia mifano katika mipaka ya alfabeti A-M, utafiti huu umeweza kuthibitisha kuwa tafsiri potovu inajitokeza katika maneno kadhaa ambayo yametafsiriwa visivyo kutoka lugha ya Kiingereza na kuonyeshwa kama tafsiri sahihi ya Kiswahili katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Imedhihirika kuwa tafsiri potovu ina maneno ya kupotosha wale wanaotegemea kamusi-tafsiri za mtandaoni katika kufanya kazi zao mbalimbali au wale wanaojifunza lugha ya Kiswahili na hivyo basi, tafsiri hii potovu si ya kutegemewa. Tafsiri hizo potovu zinazotokana na mwendelezo wa maneno ama matumizi ya kongoo isiyofaa na hivyo kusababisha maneno hayo kupoteza maana ya neno-tafsiri ama neno lake la Kiingereza.

Tumeona kuwa nadharia hupendekeza mchakato wa kufanya tafsiri ambao ikiwa utazingatiwa na wafasiri wa kamusi-tafsiri za mtandaoni basi, tafsiri bora zaidi ya maneno kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili itaafikiwa.

### 5.3.2 Vyanzo vya Tafsiri Potovu kwenye Kamusi za Mtandaoni

Sura ya tatu iliangazia vyanzo mbalimbali vya tafsiri potovu na kubainisha kuwa vyanzo hivyo hutokana na mambo mbalimbali na kuwa vyanzo hivyo vina mchango mkubwa katika tafsiri potovu ya kamusi-tafsiri za mtandaoni. Tumeona kuwa

nadharia ambayo hupendekeza mchakato fulani wa kufanya tafsiri ambao unaonekana kupuuzwa na wafasiri wa kamusi za mtandaoni. Wafasiri wa kamusi-tafsiri za mtandaoni wanafasili maana ya tafsiri ya maneno kwa kuegemea tu kwa mojawapo ya nadharia ama vipashio vya maana katika lugha ambavyo ni neno na sentensi badala ya kufasiri wakitilia maanani nadharia zote zinazochunguza maana ya neno. Malangwa (2019) anaeleza kuwa nadharia zinazochunguza maana ya maana kama vile maana kama urejeshi, maana kama dhana, maana kama utabia, maana kama ukweli na maana kama matumizi sharti zizingatiwe katika tafsiri. Utafiti huu umebaini kuwa ikiwa watafsiri watazingatia kanuni za kutafsiri basi wataepukana na mambo yanayosababisha tafsiri potovu katika kamusi-tafsiri za mtandaoni.

### 5.3.3 Mikakati ya kuboresha tafsiri bora inayoweza kutumika katika kamusi za mitandaoni

Katika sura ya nne, lengo la tatu na la mwisho ambalo ni mikakati ya kuboresha tafsiri bora inayoweza kutumika katika kamusi-tafsiri za mitandaoni lilichanganuliwa kwa misingi ya nadharia zilizotumika katika utafiti huu kwa kutumia vigezo vya kiisimu vya mofolojia, sintaksia na pragmatiki. Majibu ya hojaji pamoja na mahojiano yalitoa mapendekezo ya mikakati ambayo inaweza kuboresha kamusi-tafsiri za mitandaoni. Utafiti huu ulibaini kuwa ili kuwa na tafsiri bora ya kamusi-tafsiri za mitandaoni, kuna haja ya kubuniwa na kufuatwa kwa sera fulani kama vile kubuniwa kwa sera ya kuhakiki kamusi-tafsiri za mtandaoni, udurusu wa kongoo- matini kufanywa kwa ufasaha, kujumuisha wataalamu wa lugha katika maandalizi ya kongoo-matini, ujumuishaji wa maneno na misamiati mipya mara kwa mara, ujumuishaji wa idara ya lugha vyuoni katika kuandaa kongoo matini,

udurusu wa kamusi–tafsiri mitandaoni kufanywa mara kwa mara, na kutathmini utendakazi wa kikagua tahajia mara kwa mara, na kuongeza nguvu-kazi ya wahariri. Iwapo mikakati hii itazingatiwa, basi kamusi-tafsiri za mtandaoni zitakuwa na manufaa bora zaidi kwa watumizi wake pamoja na kuepuka kuwapotosha wale wasiojua Kiswahili na ambao wanatumia maneno yaliyotafsiriwa visivyo kwa kuwa na imani kuwa tafsiri hiyo ni bora.

### 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Pendekezo la kwanza ni kuwa Idara za Lugha ya Kiswahili vyuoni humu nchini ziweze kuhusishwa katika utafiti wa lugha ambapo wanaohusika wanaweza kutoa mchango wao kuhusi tafsiri bora zaidi inayoweza kutumika kama kongoo katika kamusi-tafsiri za mtandoni. Kwa kuwa idara hizi zinahusisha wanafunzi na wataalamu wa lugha ya Kiswahili kama vile wahadhiri, wakihusishwa basi watatoa mchango wa kimsingi sana na kuboresha kamusi hizi. Kwa upande mwingine, kitengo kinachojihusisha na teknolojia ya Lugha na Isimu-Kompyuta kinaweza kuanzishwa vyuoni humu na kuanzisha miradi yao ya kiteknolojia inayoegemea haswa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Vyuo hivi vinaweza kupewa mwongozo na vyuo vikuu vya Ughaibuni kama vile Chuo Kikuu cha Helsinki, chuo Kikuu cha Uingereza na kadhalika vilivyopiga hatua katika maswala haya. Serikali inaweza ikahusishwa ili kusaidia katika kutimiza mahitaji ya bajeti ambayo huenda ikahitajika.

Kongoo pana zaidi ya Kiswahili inaweza kuundwa na kuhusisha taasisi za Utafiti katika uundaji wake, walimu tajika wa Kiswahili, waandishi na wataalamu wa lugha hii kwani Kiswahili ni lugha inayokua kila uchao. Hali hii inaweza kusaidia kukuza kamusi-tafsiri ambazo hazijapitwa na wakati kwani zitasheheni maneno na istlahi

zinazotumika kila wakati. Kongoo ni raslimali ya thamani sana ambayo ndiyo uti wa mgongo katika utafiti wa teknolojia ya lugha na hivyo kuna haja ya kuipanua.

Wataalamu na watafiti wa lugha ya Kiswahili wanastahili kupewa mafunzo kabambe kupitia vikao vya semina na makongamano ya lugha ili wajipige msasa katika matumizi ya programu za kikompyuta kama vile kamusi na vitabu vingine. Mikutano kama hii itawezesha wataalamu hawa kujitosa kimasomaso katika maswala ya teknolojia ya lugha na kuwacha kutegemea mbinu za kimapokeo na vitabu asilia tu kwani tuko katika karne ambayo mambo ya kiteknolojia yanazidi kupiku mbinu za kiasilia za usomaji, ujifundishaji na utafiti. Wakiwa na maarifa haya, watawacha kuwategemea wataalamu wa kiteknolojia katika uchanganuzi wa data ya lugha.

Wakati wa kuandaa kamusi za mtandaoni na programu zingine, nadharia za Ismu zizingatiwe ili ziweze kutoa mwongozo na kuhakikisha kuwa kamusi–tafsiri au vitabu vingine vya kimtandao havina nafasi ya kukoselewa kwa misingi ya nadharia hii.

Watafiti wa lugha na taasisi za utafiti wa lugha zishirikishe mashirika ya uchapishaji wa vitabu vya lugha nchini kwani mashirika haya yana hazina kubwa mno ya kongoo kupitia kwa vitabu wanavyovichapisha kila mwaka. Mashirika haya bila shaka yatakuwa na kongoo iliyopigwa msasa na hivyo iwapo kongoo hii itahitajika katika ujenzi wa kamusi-tafsiri, basi itaweza kupunguza upotovu kwa asilimia kubwa.

Wanaotayarisha mitaala nchini kama vile Taasisi ya Ukuzaji Mitaala humu nchini Kenya (KICD) wanastahili kuhusishwa katika ujenzi wa kongoo ya lugha ili ujenzi

wa vitabu vya mtandaoni ikiwemo kamusi-tafsiri uwe umejikita katika vigezo vya lugha vinavyostahili na kukubalika. Taasisi kama hizi pia zitakuwa za manufaa sana katika kutoa maneno na istilahi anuai za Kiswahili zinazoaminika na kukubalika kinadharia.

Kisha, utafiti unapendekeza kuwa vyuo vikuu vya humu nchini vijizatiti na kuanzisha miradi kama hii ya uundaji wa kongoo ya kamusi za mtandaoni badala ya kuwachia mashirika na vyuo vya kigeni, ambavyo Kiswahili si lugha yao asilia.

Mbali na uundaji na tathmini ya kamusi za mtandaoni, matumizi ya Kiswahili katika uwanja wa kidijitali bado yana maeneo mengi mno ambayo yanaweza yakatafitiwa baadaye. Mwisho kabisa, utafiti umehitika na kutoa mapendekezo kwa tafiti zijazo haswa zile zinazojihusisha na maswala ya ukusanyaji na uhifadhi wa kongoo-matini.

**5.5 Hitimisho**

Sura hii imekuwa kilele cha utafiti huu ambapo imesheheni suala la utafiti ambalo ni ubora wa tafsiri katika kamusi-tafsiri za mtandaoni. Misingi ya nadharia ya isimu kongoo na ile ya tafsiri ya ulinganifu wa kimuundo imetumika katika kuchanganua malengo ya kwanza na pili ambayo ni tafsiri potovu na vyanzo vya tafsiri potovu kwa kulinganisha na kulinganua kongoo matini ya Kiingereza na Kiswahili kwa kutumia vigezo vya kiisimu vya mofolojia, sintaksia na pragmatiki. Vile vile, utafiti huu umechanganua mikakati ya kuboresha kamusi-tafsiri za mtandaoni kwa misingi ya nadharia hizi mbili. Mwisho, matokeo na mapendekezo ya utafiti huu yamewekwa bayana. Endapo mapendekezo ya utafiti huu yatatekelezwa yatawafaa watafiti wa masuala ya kamusi za mtandaoni na Kiswahili kwa jumla.

## MAREJELEO


Ahmed, E., Babusa, H., Suleiman A. (2013).*Kamusi Teule ya Kiswahili*: East African Educational Publishers, Kenya.

Bryman, A. (2008). *Social Research Methods: Population, Samples and Validity*.Texas, University of Texas.

Ekštein, K. (Ed.). (2019). *Text, Speech, and Dialogue: 22nd International Conference, TSD 2019, Ljubljana, Slovenia, September 11–13, 2019, Proceedings* (Vol. 11697). Springer Nature.

Finch, G. (2016). *Linguistic Terms and Concepts*. London: Macmillan Education, Limited

Halliday, M. A. K., & Matthiessen, C. M. (1985). An introduction to functional grammar.edward arnold, london. *Australian Rev. Appl. Linguist*, *10*(2), 163-181.

Hybels, S. & Weaver, L. (1989). *Communicating Effectively*. New York: McGraw-Hill

Ipara, I. & Maina G. (2008). *Fani ya Isimu jamii kwa Shule za Sekondari*. Oxford University Press East Africa Limited. Nairobi.

Jilali K. (2014). Ujanibishaji wa Office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu katika: Kioo cha Lugha. *University of Dar es Salam Journal*. Toleo la Kwanza, Juzuu ya 5, uk 70-99, Dar es Salam, TUKI.

Kaviti, M. (2005). *Makosa ya Kisintaksia Katika Makala Magazetini*.Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kombo, D. & Tramp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication.

Krejcie, R. & Morgan, D. (1970). Determining Sample Size for Research Activities.*Educational and Psychological Measurement.*

Leech, G. (1992). *Corpus Linguistics Approach: A word Framework for Translation Studies Research.*TranslationDictionary.com.

Leonard, M. & Pendo, S. Malangwa (2019). *Semantiki.*Nairobi:Longhorn Publishers

Mabeya, M. (2012). *Uzalishaji wa Msamiati katika mradi wa Microsoft East Africa 2004-2009'*, Tasnifu ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mahlberg, M. (2005).*English General Nouns: A Corous Theoretical Approach*. Joybrato Mukherjie. Justus Liebig University. Giessen.

Melkote, S. R. (2003). Theories of development communication. *International and development communication: A 21st-century perspective*, 129-146.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa isimu: Fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mwangi, Iribe. (1996). A Synchronic Segmental Morphophonology of Standard Kiswahili.

Nida, E. A. (1964). Towards a Science of Translating: With Special Reference to Principles and Procedures Involved in Bible Translating. Leiden: Brill.

Onwuegbuzie, A. J., & Leech, N. L. (2004). Enhancing the interpretation of “significant” findings: The role of mixed methods research. *The qualitative report*, *9*(4), 770-792.

Sinclair, J. (1982). *Somerecent Trends in The Study of Language Development.*https://journals.sagepublication.com

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Fomu Ya Kushiriki Utafiti Kwa Hiari

### SEHEMU A: MAELEZO KUHUSU UTAFITI

Mimi ni Winnie O. Lukungu, mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti kuhusu 'Ubora wa Tafsiri katika Kamusi-tafsiri za mtandaoni.' Ninakusudia kubainisha makosa ya kitafsiri ya baadhi ya maneno ili kamusi za aina hii ziwe na manufaa zaidi kwa watumizi wake kwa kupeana mapendekezo ya maneno mbadala kama tafsiri bora.

Hivyo basi, naomba ushirikiano wako wa hiari kupitia mahojiano ili kuniwezesha kuafikia malengo yangu. Utafiti huu hauna madhara yoyote kwa yule atakayeshiriki wala hakuna manufaa ya kifedha yanayoambatana nao. Habari zozote za moja kwa moja zinazohusiana na utafiti huu zitalindwa kulingana na kanuni za kuhifadhi siri ya mtafitiwa.

### SEHEMU B: KUKUBALI KUSHIRIKI

Nimesoma fomu hii na kuelewa habari yote inayohitajika kuhusu utafiti huu iwapo nitashiriki. Nimepata majibu ya maswali yote yanayohusu kushiriki kwangu katika utafiti huu. Ninaelewa kuwa kwa wakati wowote ninaweza kujitoa katika utafiti huu pasi na kutoa sababu ya hatua hii. Kwa hivyo ninakubali kushiriki kwa hiari.

Sahihi …………………………    Tarehe……………………………

**Kiambatisho II: Hojaji Kwa Watumiaji Wa Kamusi-Tafsiri**

Hojaji hii ya hiari inanuia kumsaidia mtafiti kukusanya data katika utafiti wake wa Ubora wa Tafsiri katika Kamusi- Tafsiri za Mtandaoni. Majibu yake yatamwezesha kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ushirikiano wako utatufaa. Asante.

**Maswali:**

1. Unafanya kazi gani?

   a) Mhadhiri ☐ b) Mwandishi ☐

   c) Mwalimu ☐ d) Nyingine……………………..

2. Je, unatumia kamusi –tafsiri za mtandaoni kwa malengo au shughuli gani? Ulisaidika vipi ? Eleza.

   ---------------------------------------------------------------------------------------

   ---------------------------------------------------------------------------------------

   ---------------------------------------------------------------------------------------

3. Ikiwa hutumii kamusi hizi ilhali inaweza kuhusiana na taaluma yako, eleza kwa nini

   ___

   Unaweza kukadiria vipi ubora wa kamusi hizi kiasilimia kulingana na manufaa uliyopata kwayo?

   a) 70 -100% ☐ b) 40- 70% ☐ c) Chini ya 40 ☐

4. Je, unahisi kuwa kamusi hizi zinakidhi mahitaji yako kama mtumiaji wa lugha ya Kiswahili? Kwa nini?

-----------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

5. Umekumbana na matatizo yepi katika kutumia kamusi hizi? Wewe hutatua vipi matatizo haya?

-----------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

6. Unafikiria kuwa matatizo haya hutokana na nini? Eleza.

-----------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

7. Toa mapendekezo yako ya kuboresha kamusi hizi.

-----------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

8. Kuna jambo lingine la ziada linalohisiana na utafiti huu ambalo ungependa kudokezea?

-----------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

**MWISHO, ASANTE SANA.**

**Kiambatisho III: Hojaji Kwa Mtaalamu Wa Teknolojia**

Hojaji hii ya hiari inanuia kumsaidia mtafiti kukusanya data katika utafiti wake wa Ubora wa Tafsiri katika Kamusi- Tafsiri za Mtandaoni. Majibu yake yatamwezesha kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ushirikiano wako utatufaa. Asante.

**Maswali:**

1. Programu za kamusi ya mtandaoni huchukua kadri ya muda gani kuwa tayari?

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

2. Hatua au mchakato wa kuandaa program hizi ni upi?

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

3. Changamoto zipi huzuka katika kuandaa programu hizo

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

   ------------------------------------------------------------------------------------------

4. Makosa yanayodhihirika kwenye programu hizi huweza kutokana na nini?

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------

5. Kwa maoni yako, programu hizi zinaweza kuboreshwa kwa njia gani?

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

6. Je, una la ziada lenye manufaa kwa utafiti huu?

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

**MWISHO, ASANTE**

## Kiambatisho IV: Barua Ya Chuo Ya Ruhusa Ya Utafiti

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 7th June, 2022

TO: Winnie O. Lukungu
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

REF: C50/OL/CTY/34129/2016

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 25th May, 2022 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Ubora wa Tafsiri Inayodhihirika Katika Kamusi Tafsiri za Mtandaoni".

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

ELIJAH MUTUA
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Dr. Boniface Ngugi
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

EM/lnn

## Kiambatisho V: Idhini Ya NACOSTI

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/OL/CTY/34129/2016

DATE: 7th June, 2022

Director General,
National Commission for Science, Technology and Innovation
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR WINNIE O. LUKUNGU - REG. NO. C50/OL/CTY/34129/2016.

I write to introduce **Winnie O. Lukungu** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili & African Languages.**

Winnie intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, **"Ubora wa Tafsiri Inayodhihirika Katika Kamusi Tafsiri za Mtandaoni".**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

PROF. ELISHIBA KIMANI
AG. DEAN, GRADUATE SCHOOL

*EM/lnn*